JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MKUTANO NA WAANDISHI WA HABARI: MAELEZO YA KATIBU MKUU –WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI JUU YA MAFANIKIO YA UONGOZI WA SERIKALI YA AWAMU YA NNE KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE

(DESEMBA, 2005 - DESEMBA 2009)

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI
P.O.BOX 9111
DAR ES SALAAM
MACHI, 2010

1. UTANGULIZI

Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne yametokana na Wizara ya Fedha na Uchumi kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA); Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs); na Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya 2005. Pamoja na madhara ya msukosuko wa uchumi wa dunia, utekelezaji wa malengo hayo umekuwa na mafanikio makubwa katika maeneo yanayosimamiwa na Wizara. Mwenendo wa uchumi jumla katika kipindi cha mwaka miaka yote minne (2005-2009) umeendelea kuimarika licha ya kukabiliwa na changamoto ukosefu wa mvua katika baadhi ya maeneo ya nchi, kupanda kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia mwaka 2008, athari za msukosuko wa kiuchumi duniani, nk.

2. DIRA NA DHIMA YA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

Wizara ya Fedha na Uchumi imejipanga kutoa huduma kwa ufanisi wa hali ya juu ili kuongoza juhudi za Serikali za kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Ili kutekeleza hayo, Wizara ya Fedha na Uchumi imejiwekea Dira ya kuwa taasisi inayoongoza jitihada za kuwa na ukuaji uchumi ambao ni endelevu na unaozingatia usimamizi bora wa rasilimali fedha za Umma. Hivyo, Dhima ya Wizara ni kuhakikisha kuwepo na uchumi endelevu kwa kubuni sera sahihi za fedha na za kibajeti na kukuza dhana ya matumizi ya Teknologia ya habari na Mawasiliano (ICT) katika usimamizi wa uchumi.

3. MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

Ili kufanikisha Dhima na Dira kama ilivyoelezwa hapo juu, Wizara ya Fedha na Uchumi ina majukumu yafuatayo:

i. Kuchambua na kubuni Sera za Uchumi Jumla;
ii. Kuratibu na kusimamia shughuli za kiuchumi pamoja na kuandaa miongozo ya uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji;
iii. Kuweka mazingira bora ili kuwezesha sekta binafsi kushamiri na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii;
iv. Kuibua na kubainisha fursa za kuvutia uwekezaji;
v. Kuandaa na kusimamia sera za mapato na matumizi ya Serikali;
vi. Kuandaa na kusimamia sera za madeni na mkakati wa kuyadhibiti;
vii. Kuandaa na kusimamia sera za fedha na urari wa malipo na nchi za nje;
viii. Kusimamia takwimu zote zinazohusu Uchumi na Sekta ya Fedha;
ix. Kuratibu utekelezaji wa MKUKUTA;

x. Kusimamia matumizi ya fedha za Umma;na
xi. Kudhibiti Fedha Haramu na Ufadhili wa Vitendo vya Kigaidi.

4. ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2005

Wizara ya Fedha na Uchumi, pamoja na taasisi zilizo chini yake inaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 kama ilivyoainishwa katika chapisho lake la Agosti 2005. Aidha, katika kutekeleza hayo, Wizara imeongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA) na Sera za Fedha na maelekezo mengine ya Serikali.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 imelenga kuipeleka Tanzania katika kundi la Nchi za Kipato cha Kati (middle-income countries), kutoka ilipo hivi sasa ya Nchi ya Kipato cha Chini (low-income country) ifikapo mwaka 2025. Malengo ya Dira yamewekwa katika makundi makubwa mawili, yaani uchumi imara na unaokua na hali bora ya maisha ya Watanzania wote. Kulingana na matarajio ya DIRA, Tanzania ya mwaka 2025 inatarajiwa kuwa ni Taifa lenye sifa kuu tano:

i. Maisha bora ya jamii na uwezo wa kipato;
ii. Amani, utulivu na umoja;
iii. Utawala bora;
iv. Jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi; na
v. Uchumi wenye uwezo wa ushindani na wenye ukuaji endelevu kwa maslahi ya watu wote.

Malengo ya Maendeleo ya Milenia

Taarifa hii imezingatia utekelezaji wa Malengo ya Milenia (MDGs) -2015, ambapo malengo yake makuu nane ni yafuatayo:

1. Kuondoa umaskini uliokithiri na njaa;
2. Kufanikisha elimu ya msingi kwa wote (UPE);
3. Kuwepo fursa sawa kwa kijinsia zote na kuwawezesha zaidi wanawake;
4. Kupunguza vifo vya watoto;
5. Kuboresha afya ya uzazi;
6. Kupambana dhidi ya Virusi vya UKIMWI/UKIMWI, Malaria na magonjwa mengine
7. Kuhakikisha utunzaji endelevu wa mazingira; na
8. Kukuza ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya maendeleo.

Kulingana na **Ilani ya Uchaguzi**, Wizara inatakiwa kujikita katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kusimamia Uchumi Jumla

(ii) Kusimamia Bajeti ya Serikali
(iii) Kuzipatia rasilimali fedha Sekta zifuatazo:
- Sekta za Kijamii
- Sekta za Uzalishaji
- Sekta ya Mawasiliano na Miundombinu

(iv) Kuboresha Sekta Ya Fedha
- Usimamizi wa Sekta ya Fedha
- Kuwezesha Upatikanaji wa Mikopo
- Kuwawezesha wajasiriamali

(v) Kuboresha huduma kwa wastaafu.
(vi) Kuimarisha Mashirika ya Umma/Ubinafsishaji

5. MAFANIKIO YA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI KATIKA KUTEKELEZA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2005

Wizara ya Fedha na Uchumi, pamoja na taasisi zake katika kipindi cha Desemba 2005 hadi Desemba, 2009 imefanikisha mengi katika ahadi mbalimbali zilizotolewa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kama ifuatavyo:-

5.1 USIMAMIZI WA UCHUMI JUMLA

Katika usimamizi wa Uchumi Jumla, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 imebainisha malengo yafuatayo:

(i) Kukuza uchumi kwa kiwango cha asilimia 10 kwa mwaka ifikapo 2010 kutoka ukuaji wa mwaka 2005 wa asilimia 6.7
(ii) Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa, wa Taifa linalojitegemea.

Utekelezaji

(i) Ukuaji wa Uchumi

Katika kipindi cha miaka minne (2005 – 2008) uchumi umeendelea kuimarika na Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 7.2 kwa mwaka katika kipindi hicho. Ukuaji huu wa uchumi ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi katika sekta za: Bidhaa za viwanda; ujenzi; fedha; na mawasiliano na uchukuzi. Sekta ya mawasiliano ndio inayoongoza katika kuwa na viwango vya juu vya ukuaji kwani katika kipindi hicho sekta hii ilikua kwa wastani wa asilimia 19.6 kwa mwaka.



Pamoja na mwaka 2009 kuwa ni mwaka ambao kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa inatarajiwa kupungua kutokana na athari za msukosuko wa uchumi wa dunia, takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka zinaonesha kuwa, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka (Januari – Machi 2009) uchumi wa Taifa ulikua kwa asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 6.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2008. Aidha, ukuaji wa uchumi katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka (Aprili – Juni 2009) ulikuwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 7.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2008. Kulingana na mwenendo huu, matarajio ya kukua kwa uchumi kwa mwaka 2009 ni kufikia zaidi ya makisio ya awali ya asilimia 5.0.

(ii) Pato la Kila Mtanzania (Per Capita Income)

Mwaka 2008, Pato la Taifa lilikuwa sh. 24,781,679 milioni kwa bei za mwaka husika au sh.14,828,345 milioni kwa bei za mwaka 2001. Kutokana na idadi ya watu Tanzania Bara kukadiriwa kuwa milioni 39.3, Pato la wastani la kila mtu lilikuwa sh. 628,259 mwaka 2008 ikilinganishwa na sh.548,388. mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 14.8. Kwa Dola za Kimarekani Pato la Wastani kwa Kila Mtanzania liliongezeka kutoka Dola 444.8 mwaka 2007 hadi Dola 525.2 mwaka 2008. Kwa kuzingatia takwimu hizi Pato la Mtanzania limekuwa likiongezeka katika kipindi chote cha awamu ya nne kutoka Dola za Kimarekani 392.8 mwaka 2005 hadi dola 525.2 mwaka 2008.

Mwenendo wa Pato la Mtanzania (Per Capita Income) 2005 -2009					
Kiashiria	**2005**	**2006**	**2007**	**2008**	**2009***
Jumla ya Pato la Taifa (GDP mp)	15,965,294.0	17,941,268.0	20,948,403.3	24,781,679.4	28,060,519.1
Thamani ya Shillingi	1,122.7	1,251.9	1,232.8	1,196.3	1,319.0
Idadi ya Watu (Tanzania)	37,267,529.0	38,669,744.0	39,445,999.0	40,667,726.0	41,915,799.0
Pato la Wastani la Mtanzania (Tshs)	441,030.2	478,433.8	546,955.7	629,884.4	682,737.7
Pato la Wastani la Mtanzania (USD)	392.8	382.2	443.7	526.5	517.6

* *Takwimu za Mwaka 2009 ni za makadirio*.

Idadi ya Watu na Maendeleo

Tatizo la ongezeko la idadi watu Tanzania ni changamoto kubwa katika kuleta maendeleo. Pamoja na kuwa na ongezeko la idadi ya watu nchini inakadiriwa kuwa kasi ya ongezeko inapungua mwaka hadi mwaka. Makadirio ya idadi ya watu kwa kutumia takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 yanaonyesha kuwa mwaka 2005, Tanzania ilikuwa na watu wapatao 37,267,530 wakati ambapo mwaka 2009 idadi ya watu nchini ilikadiriwa kuwa watu 41,915,799. Pamoja na ongezeko la jumla (absolute number), kiwango cha ukuaji wa ongezeko hilo kinakadiriwa kupungua. Mwaka 2002, kulingana na Sensa ya Watu na Makazi kiwango cha ukuaji wa watu kilikadiriwa kuwa 2.9 asilimia wakati ambapo inatarajiwa kuwa ifikapo mwaka mwaka 2025 kiwango hicho kuwa ni asilimia 2.5. Kwa upande wa makazi, takwimu za makadirio za sensa zinaonyesha kuwa watu wengi wanaoishi mijini wameongezeka kwa kutoka asilimia 23.0 mwaka 2005 hadi asilimia 25.6 mwaka 2008.

Hadi kufikia Decemba 2008, mtawanyiko wa watu (population density) unaonyesha kuwa mkoa wenye idadi kubwa zaidi wa watu ni Dar es Salaam, ambao una watu 2,114 kwa kila kilometa mraba, ikifuatiwa na Mwanza uliokuwa na watu 172 kwa kila kilometa mraba, Arusha watu 119 kwa kila kilometa mraba na Mara watu 86 kwa kila kilometa mraba. Mkoa uliokuwa na kiwango kidogo zaidi cha msongamano wa watu ulikuwa ni Lindi, ambao ulikuwa na watu 13 kwa kila kilometa mraba ukifuatiwa na Ruvuma na Rukwa ambayo ilikuwa na watu 21 kwa kilometa mraba kila mmoja.

Serikali itaendelea na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu kwa ajili ya kutatua changamoto zinazotokana na ongezeko la idadi ya watu na rasilimali zilizopo kupitia programu mbali mbali na kutoa elimu juu ya masuala ya watu na maendeleo. Jedwali hapo chini ilinaonyesha idadi wa watu Tanzania.

JUMLA YA IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA: 2005-2009

Mkoa	2005	2006	2007	2008	2009**
Dodoma	1,786,073	1,896,786	1,951,071	2,004,544	2,058,630
Arusha	1,427,904	1,475,489	1,522,975	1,570,394	1,617,728
Kilimanjaro	1,435,847	1,503,014	1,535,975	1,569,212	1,602,530
Tanga	1,716,271	1,753,284	1,837,661	1,880,389	1,923,468
Morogoro	1,881,113	1,929,087	1,975,160	2,021,713	2,068,426
Pwani	944,145	968,637	991,586	1,014,968	1,038,654
Dar es Salaam	2,799,241	2,801,675	2,881,548	2,961,150	3,040,118
Lindi	816,815	851,764	869,522	887,434	905,480
Mtwara	1,176,112	1,220,248	1,246,089	1,271,912	1,297,751
Ruvuma	1,192,680	1,235,161	1,268,738	1,303,330	1,338,800
Iringa	1,553,392	1,617,696	1,649,200	1,679,828	1,709,225
Mbeya	2,201,206	2,346,388	2,423,635	2,502,258	2,581,792
Singida	1,150,367	1,222,810	1,258,545	1,294,584	1,330,931
Tabora	1,887,507	2,004,115	2,086,048	2,170,926	2,258,664
Rukwa	1,251,697	1,302,278	1,349,579	1,398,866	1,450,118
Kigoma	1,910,592	1,970,750	1,601,020	1,669,078	1,740,111
Shinyanga	3,060,176	3,277,784	3,411,023	3,549,342	3,692,941
Kagera	2,206,814	2,210,217	2,293,093	2,379,637	2,469,904
Mwanza	3,196,714	3,168,904	3,265,729	3,364,378	3,464,566
Mara	1,461,270	1,572,068	1,631,031	1,692,449	1,756,442
Manyara	1,141,376	1,198,051	1,241,994	1,288,280	1,337,015
Tanzania Bara	**36,197,312**	**37,526,206**	**38,291,222**	**39,474,672**	**40,683,294**
Kaskazini Unguja	146,221	155,066	160,175	165,544	171,150
Kusini Unguja	99,678	103,191	105,456	107,811	110,183
Mjini Magharibi	441,446	461,759	447,716	459,502	471,341
Kaskazini Pemba	196,221	216,174	224,951	234,142	243,759
Kusini Pemba	186,651	207,348	216,479	226,055	236,072
Zanzibar	**1,070,217**	**1,143,538**	**1,154,777**	**1,193,054**	**1,232,505**
Tanzania	**37,267,529**	**38,669,744**	**39,445,999**	**40,667,726**	**41,915,799**

Chanzo: Wizara ya Fedha na Uchumi
** Makadirio kulingana na takwimu za matokeo ya sensa mwaka 2002

(iii) Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei umekuwa ni moja ya changamoto za kujenga uchumi imara lakini hali imeendelea kuimarika na kasi ya upandaji bei kwa bidhaa muhimu imeendelea kudhibitiwa kwa kiwango cha kuridhisha. Udhibiti huu umefanyika kwa umakini kwa kutumia sera sahihi za bajeti na za fedha.

Katika kipindi cha miaka minne iliyopita kasi ya ongezeko la bei imekuwa ikiongezeka kwa mwaka. Mfano katika kipindi cha mwaka 2005, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 5.0 na kuongezeka hadi kufika asilimia 10.3 mwaka 2008. Hadi kufikia mwezi Desemba 2009, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 12.2 ikilinganishwa na asilimia 13.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2008. Kwa wastani mfumuko wa bei ulipanda kwa kiwango cha tarakimu mbili katika mwaka 2008 kutokana na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia kulikopelekea kuwa na kiwango cha juu zaidi hadi kufikia Dola za Kimarekani 150 kwa pipa moja la mafuta ghafi. Aidha, katika mwaka 2008 nchi yetu ilikumbwa na ukame katika baadhi ya maeneo na hivyo kusababisha ukosefu wa chakula na bei zake kupanda. Kutokana na hali hiyo mfumuko wa bei ulifikia kiwango cha juu

cha asilimia 13.5 desemba 2008. Hata hivyo, kutokana na juhudi zilizochukuliwa mfumuko wa bei umeanza kurudi chini hadi kufikia asilimia 10.9 Januari 2010.

Itakumbukwa kwamba, chakula huchangia asilimia 55.9 katika matumizi yote ya kaya, na hivyo upatikanaji wa chakula nchini ni muhimu ili kusaidia kushusha mfumuko wa bei. Hata hivyo, kuanzia mwezi Oktoba 2009, kasi ya upandaji bei ya chakula imeanza kushuka, kutoka ongezeko la asilimia 18.1 hadi asilimia 14.5 mwezi Desemba 2009. Serikali imedhamiria kujenga Uchumi wa kisasa kwa kujenga Taifa linalojitegemea na kuboresha sekta zote za uchumi na maendeleo ya jamii. Kuhimiza na kuleta mapinduzi ya kilimo cha kisasa, ni moja ya mikakati ya kujenga taifa lenye uchumi imara na Serikali imedhamiria kufikia lengo hilo kupitia msukumo mpya wa Kilimo Kwanza.

Ujazi wa Fedha na Karadha

Katika mwaka 2009, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 20.8 ikilinganishwa na asilimia 24.4 mwaka 2008. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)1 ulikua kwa 18.4 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 22.7 mwaka 2008. Kasi ndogo ya ongezeko la ujazi wa fedha ilitokana na ongezeko dogo la utoaji mikopo kwa sekta binafsi kutokana na tahadhari iliyochukuliwa na benki kufuatia hali ya mtikisiko wa masoko ya fedha na mitaji duniani. Kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ilipungua kutoka wastani wa asilimia 35.8 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita hadi wastani wa asilimia 27.9 mwaka 2009.

Uzaji wa Fedha- Kwa kipindi cha 2005 hadi 2008 - Tsh Milioni

Uzaji wa Fedha-	Kipindi kinachoishia June 2008			
	2005	2006	2007	2008
Ujazi wa fedha, maana finyu zaidi (M0)*	**24.5%**	**16.2%**	**22.6%**	**21.2%**
Amana za hundi	33.3%	20.5%	17.5%	39.3%
Ujazi wa fedha, maana finyu (M1)	**28.9%**	**18.4%**	**19.9%**	**30.6%**
Amana za muda maalum	22.1%	43.6%	14.3%	54.0%
Amana za akiba	26.9%	48.3%	24.6%	18.0%
Ujazi wa fedha, maana pana (M2)	**27.5%**	**28.4%**	**20.2%**	**30.8%**
Amana za fedha za kigeni	20.5%	52.1%	21.8%	5.2%
Ujazi wa fedha, maana pana zaidi (M3)	**25.5%**	**34.9%**	**20.7%**	**22.8%**
Akiba halisi ya mali za kigeni (Foreign Assets	**6.8%**	**27.9%**	**16.1%**	**3.7%**
Amana Halisi Nchini	**110.6%**	**51.1%**	**29.8%**	**55.9%**
Karadha Nchini	33.9%	62.2%	14.2%	27.1%
Mikopo kwa serikali	80.6%	156.3%	-38.3%	-65.6%
Mikopo kwa sekta isiyo serikali	26.2%	40.2%	36.6%	45.0%
Amali halisi nyinginezo (net other items)	-21.1%	83.3%	-10.4%	-38.4%

[1]M3 = M2 + Amana za fedha za kigeni
M2 = M1 + Amana za muda maalumu + Amana za akiba
M1 = Fedha zilizo kwenye mzunguko nje ya mabenki + Amana za hundi

Mwenendo wa Riba

katika miaka ya hivi karibuni, viwango vya riba vimeonesha mwelekeo mzuri hasa kuanzia mwaka wa fedha 2006/07, ambapo riba kwenye amana za akiba zimekuwa zikiongezeka, wakati riba zinazotozwa kwenye mikopo zimekuwa zikipungua. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2009/10 wastani wa viwango vya riba kwa amana za akiba za muda mfupi (hadi mwaka mmoja) ulikuwa asilimia 8.92 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.21 katika mwaka wa fedha 2003/04. Katika kipindi hicho, wastani wa viwango vya riba vilivyotozwa na benki za biashara kwa mikopo ya mwaka mmoja ulipungua hadi asilimia 13.93 kutoka asilimia 15.75. Kutokana na mwelekeo huo wa riba, tofauti kati ya viwango vya riba kwenye amana za mwaka mmoja na viwango vya riba kwenye mikopo ya mwaka mmoja ilishuka kutoka 10.54 mwaka 2003/04 hadi 5.01 mwaka 2009/10, sawa na kushuka kwa asilimia 47.5. Jedwali hapo chini ilinaonesha mwenendo wa riba kutoka mwaka 2003/04 hadi mwaka 2009/10.

Table 1: Mwenendo wa Riba za Mabenki (Wastani)

	2003/04	2004/05	2005/06	2006/07	2007/08	2008/09	2009/10 (July - Dec)	Average
Riba kwenye amana za mwaka mmoja	5.21	5.94	7.26	8.78	9.50	8.60	8.92	**7.74**
Riba kwenye mikopo ya mwaka mmoja	15.75	15.54	15.65	15.23	13.95	13.67	13.93	**14.82**
Tofauti kati ya riba ya mikopo na riba ya amana	**10.54**	**9.60**	**8.39**	**6.45**	**4.45**	**5.07**	**5.01**	**7.07**
Riba kwenye amana za mwaka mmoja (Wakopaji wakuu)	6.62	7.96	9.80	9.03	10.47	10.39	10.25	**9.22**
Riba kwenye mikopo ya mwaka mmoja (Wakopaji wakuu)	8.79	10.78	11.54	11.44	12.20	12.87	13.73	**11.62**
Tofauti kati ya riba ya mikopo na riba ya amana	**2.16**	**2.82**	**1.73**	**2.41**	**1.73**	**2.48**	**3.48**	**2.40**
Riba kwenye dhamana za serikali (mwaka mmoja)	7.47	10.30	13.48	14.41	12.81	12.33	8.28	**11.30**
Riba kwenye dhamana za serikali (kiwango cha jumla)	7.33	9.17	12.39	13.48	11.24	10.56	5.40	**9.94**
Bank rate	12.29	14.14	17.09	18.34	16.30	15.31	4.89	**14.05**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Thamani ya Fedha ya Tanzania

Mwaka 2005, Wastani wa thamani ya shilingi ya Tanzania ulikuwa sh. 1,122.7 kwa dola moja ya Marekani ikilinganishwa na wastani wa sh. 1,195.75 kwa dola moja ya Marekani mwaka 2008. Kuongezeka kwa thamani ya shilingi kulitokana na kuporomoka kwa thamani ya dola ya Marekani. Thamani ya shilingi ya Tanzania ilishuka kutoka wastani wa shilingi 1,195.75 kwa dola mwaka 2008 hadi wastani wa shilingi 1,318.71 kwa dola mwaka 2009, sawa na kushuka kwa wastani wa asilimia 10.3. Kushuka kwa thamani ya shilingi kulitokana hasa na msukosuko wa fedha ulimwenguni uliowafanya wafanyabiashara kuamini kuwa fedha za kigeni zingeadimika na hivyo kutafuta dola za ziada kwa lengo la kuhodhi. Hali hiyo ya kuhodhi fedha za kigeni inadhihirika katika ongezeko kubwa la rasilimali za fedha za kigeni (foreign assets) na amana za fedha za kigeni katika benki za hapa nchini.



Ni matarajio ya Serikali kwamba, thamani ya shilingi itaimarika kadri athari za msukosuko wa uchumi zinavyopungua. Serikali inaendelea kutekeleza sera ya soko huria, ambapo thamani ya shilingi hutegemea mahitaji na upatikanaji wa fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha hizo. Hali kadhalika, Serikali inaendelea kutekeleza sera zinazolenga kuongeza mauzo nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika sekta hiyo ili kuongeza mapato katika fedha za kigeni.

Biashara ya Bidhaa Nje:

Mauzo ya bidhaa nje yaliongezeka kwa asilimia 3.2 hadi kufikia dola za Kimarekani 2,697.6 milioni mwezi Novemba 2009. Ongezeko hilo lilichangiwa na mauzo ya dhahabu kwa asilimia 9.0 hadi kufikia dola 1,023.8 milioni, tumbaku kwa asilimia 35.3 hadi kufikia dola 151.4. Aidha, mauzo ya kahawa nje yaliongezeka hadi kufikia dola 117.2 milioni, sawa na asilimia 29.0.

Uagizaji bidhaa:

Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje (fob) ilipungua kwa asilimia 7.1 mwaka 2009 kufikia dola za Kimarekani milioni 7,514.0, kutoka dola milioni 8,089.2 mwaka 2008. Hii ilitokana hasa na kupungua kwa thamani katika uagizaji wa mafuta kutoka nje.

Akiba ya Fedha za Kigeni

Mwaka 2005, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola 2,048.4 milioni sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa kwa miezi 4.8 ikilinganishwa ikilinganishwa na dola 2,869.7 milioni mwaka 2008. Kiasi hicho cha akiba ya fedha za kigeni mwaka 2008 kilikuwa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kwa miezi isiyopungua 4.6.

Hadi Desemba 2009, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Kimarekani milioni 3,551.3 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 2,872.6 mwezi Desemba, 2008. Kiasi hiki ni sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 5.6. Jedwali hapo chini ilinaonesha mwenendo wa akiba ya fedha za kigeni.

Mwenendo wa Akiba ya Fedha za Kigeni (Foreign Reserves) 2004 -2009

Kiashiria	2004	2005	2006	2007	2008	2009
Akiba ya Fedha za Kigeni (mil.USD)	2,961	2,048.4	2,260.1	2,755.2	2,872.6	3,551
Miezi ya Uagizaji	6.6	4.8	4.3	4.6	4.6	5.6

Chanzo: Wizara ya Fedha na Uchumi

6. UTEKELEZAJI WA MKUKUTA, 2005-2009

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA) unatilia mkazo suala la kukuza uchumi kama kichocheo kimojawapo katika kupunguza umasikini. Mkakati huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2005/06 – 2009/10). Mkakati huu ni mpana zaidi na unahusisha sekta zote na wadau wote wa maendeleo ikijumuisha Serikali, sekta binafsi na wananchi wote katika ngazi na jumuiya mbali mbali. Mkakati huu unatilia mkazo zaidi matokeo tarajiwa (outcome approach) ya sekta zote.

Nafasi ya Mkukuta Katika Utekelezaji wa Dira

MKUKUTA unalenga kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, mbinu yake kuu ikiwa ni kuelekeza jitihada katika kufikiwa kwa matokeo tarajiwa (outcome – oriented). MKUKUTA unalenga katika matokeo ya utekelezaji yaliyowekwa katika nguzo kuu tatu:

i. Ukuaji wa uchumi na kuondoa umasikini wa kipato;
ii. Uboreshaji wa maisha na ustawi wa jamii; na
iii. Utawala Bora na Uwajibikaji.

Katika kila nguzo kuna malengo na shabaha zilizopangwa katika utekelezaji na nguzo hizi tatu zina uhusiano mkubwa miongoni mwake.

Taarifa za utekelezaji wa MKUKUTA zimekuwa zikitolewa ikiwa ni pamoja na Taarifa ya kila Mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA (MKUKUTA Annual Implementation Report –MAIR) na Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Watu (Poverty and Human Development Report – PHDR) itolewayo kila baada ya miaka

miwili. Taarifa hizi zimekuwa msingi wa majadiliano na wadau mbalimbali na kutoa maoni yanayolenga kuleta ufanisi na kufikia malengo yanayotarajiwa.

Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato

Matokeo ya Utafiti wa Matumizi ya Kaya (Household Budget Survey 2007) yanaonesha kuwa kiwango cha umaskini kimepungua kwa wastani. Tathimini inaonesha kuwa kwa ujumla tumepunguza hali ya umasikini wa kipato nchini kutoka asilimia 35.7 (2000/01) hadi asilimia 33.3 (2007). Aidha, kumekuwepo na mafanikio katika maeneo mengine ya matumizi ya kaya hasa katika elimu na matumizi ya vyombo vya afya vya umma. Licha ya mafanikio katika maeneo haya, umaskini wa kipato hauwezi kujionesha wazi kupungua kwake katika kipindi cha muda mfupi.

Pamoja na umaskini kipato kupungua, matokeo ya utafiti wa Mapato na Matumizi ya kaya yanaonesha kuwa umiliki wa mali umeongezeka kwa kiasi kikubwa tangu mwaka 2000/01. Kwa mfano, idadi ya watu wanaomiliki simu imeongezeka kutoka asilimia 1.2 mwaka 2000/01 hadi asilimia 25 mwaka 2007. Umiliki wa vyandarua umeongezeka kutoka asilimia 37.1 hadi asilimia 68.9 kwa kipindi hicho hicho. Matumizi ya vifaa vya ujenzi wa nyumba za kudumu yameongezeka katika maeneo yote ya mjini na vijijini. Matumizi ya bati za kuezekea nyumba yameongezeka kutoka asilimia 43 mwaka 2000/01 hadi asilimia 55 mwaka 2007.

Mafanikio ya MKUKUTA I

Pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya MKUKUTA, mafanikio mbalimbali yamepatikana. Kwa muhtasari baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

(i) Ukuaji wa Pato la Taifa kwa wastani wa asilimia 7.2 kwa mwaka,

(ii) Ongezeko la mapato ya ndani kwa wastani wa shilingi 177.1 bilioni kwa mwezi, mwaka 2005/06 hadi shilingi 357.8 bilioni mwaka 2008/09;

(iii) Kuongezeka kwa kiwango halisi cha uandikishaji wa wanafunzi katika shule ya msingi kutoka 96.1 mwaka 2006 hadi asilimia 97.2 mwaka 2008. Kiwango cha ukatishaji masomo kilishuka kutoka asilimia 3.4 mwaka 2006 hadi asilimia 3.1 mwaka 2008. Aidha, kiwango halisi cha uandikishaji kidato cha kwanza hadi cha nne pia kilipanda kutoka asilimia 13.4 mwaka 2006 hadi 20.7 mwaka 2007;

(iv) Kupungua kwa vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka watoto 112 kati ya 1000 waliozaliwa hai mwaka 2004/05 hadi

kuifikia 91 kati ya 1000 waliozaliwa hai mwaka 2008. Vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka 68 kati ya watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2004/05 kufikia 58 kati ya watoto 1,000 mwaka 2008;

(v) Kupungua kwa maambukizi ya virusi vya ukimwi kutoka asilimia 7.0 mwaka 2006 hadi asilimia 5.7 mwaka 2008. Aidha, maambukizi mapya kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15-24 yanaonesha kupungua kutoka asilimia 3.5 mwaka 2007 hadi asilimia 2.4 mwaka 2008;

(vi) Kuboreka kwa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kutoka asilimia 73.0 mwaka 2006/07 hadi asilimia 83 mwaka 2008/09. Upatikanaji wa maji safi vijijini umeongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2006/07 na kufikia asilimia 58.3 mwaka 2008/09. Aidha, upatikanaji wa maji safi na salama kwa mkoa wa Dar es Salaam umeongezeka kutoka asilimia 50 mwaka 2005 hadi asilimia 68 mwaka 2008;

(vii) Kuongezeka idadi ya wanawake katika ngazi za maamuzi imefikia asilimia 29 kwa mwaka 2008.

(viii) Kuongezeka kwa uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma na kuongezeka kwa uwazi katika ugawaji wa rasilimali katika Mikoa na Halmashauri;

(ix) Kukua kwa demokrasia kwa kuendesha chaguzi mbalimbali zikiwemo za mamlaka za serikali za mitaa kwa amani na utulivu; na

(x) Kuimarisha uhuru wa maoni ya wananchi; na kuzingatia utawala wa sheria kwa kutoingilia uhuru wa mahakama.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya MKUKUTA umekabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:

i. Kushirikisha wadau binafsi na asasi za kijamii katika hatua ya kupanga mipango ya maendeleo;
ii. Kuongeza idadi ya rasilimali watu katika sekta zote na kuboresha utendaji kazi;
iii. Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma;
iv. Kuboresha huduma za jamii (elimu, afya na maji) na uwiano sawa katika ngazi zote lengo likiwa hasa ni: kuwa na elimu bora, kupunguza vifo vya mama wajawazito na kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini;
v. Kuboresha uzalishaji katika sekta ya kilimo na kusindika mazao na kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini;

vi. Kuboresha sekta miundombinu muhimu katika uchumi ikiwemo ya usafirishaji hasa reli na bandar, na upatikanaji wa nishati ya umeme;
vii. Kuimarisha mazingira ya biashara ili kuwezesha upatikanaji wa ajira binafsi; na
viii. Kuboresha upatikanaji wa huduma za mikopo ya kilimo kwa wakulima;

Mwezi Juni, 2010 ni mwisho wa utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya MKUKUTA. Changamoto zilizojitokeza katika Awamu ya kwanza zimezingatiwa katika uandaaji wa Awamu ya Pili ya MKUKUTA. Awamu ya Pili ya MKUKUTA itaendelea kuzingatia zaidi matokeo na kubaki na nguzo kuu tatu. Msukumo zaidi utakuwa katika ukuaji wa uchumi bila kuathiri huduma nyingine za kijamii. Aidha, Mkakati huu utaainisha maeneo ya kipaumbele, kuoanisha matokeo na njia za kufikia matokeo hayo.

7. UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MILENIA (MDGs) 2015

Serikali yetu ni miongoni mwa nchi wanachama wa UN zilizotiliana sahihi makubaliano ya maazimio hayo. Maazimio hayo yamegawanywa katika malengo (Goals) nane na kila lengo lina shabaha (targets) yake ya utekelezaji ambayo inatakiwa yawe yamefikiwa ifikapo mwaka 2015. Utekelezaji wa malengo haya unaendana sanjari na ule wa utekelezaji wa MKUKUTA. Malengo hayo ni:

1. Kuondoa umaskini uliokithiri na njaa;
2. Kufanikisha elimu ya msingi kwa wote (UPE);
3. Kuwepo fursa sawa kwa kijinsia zote na kuwawezesha zaidi wanawake;
4. Kupunguza vifo vya watoto;
5. Kuboresha afya ya uzazi;
6. Kupambana dhidi ya Virusi vya UKIMWI/UKIMWI, Malaria na magonjwa mengine
7. Kuhakikisha utunzaji endelevu wa mazingira; na
8. Kukuza ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya maendeleo.

Hatua Zilizofikiwa katika Utekelezaji

Malengo hayo yanalenga kutatua changamoto kuu za kimaendeleo. Kwa ujumla Tanzania ipo mbele katika utekelezaji wa baadhi ya malengo ya milenia ikilinganishwa na nchi nyingine zinazoendelea. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo nchi yetu bado inahitaji juhudi za ziada katika kufikia malengo ya milenia kwa asilimia 100. Kwa upande wa elimu kwa wote, Tanzania imekuwa ni nchi ya mfano katika eneo la uandikishaji wa watoto wanaoanza elimu ya msingi. Aidha kwa upande wa ushirikishaji wa wanawake katika ngazi za maamuzi tayari idadi

ya wanawake wanaoshiriki katika ngazi hizo imekuwa ikiongezeka katika ngazi hizo kwa kasi zaidi. Kwa mfano hadi sasa wabunge wanawake wamefikia asilimia 33 ya wabunge wote katika Bunge la Tanzania. Aidha, hali ni kama hiyo katika sekta mbalimbali. Vile vile, suala la uhifadhi wa mazingira nalo linaendelea vemaKuhusu hatua ya utekelezaji wa malengo ya Maendeleo ya Milenia. Serikali inaendelea kuhuisha mipango na bajeti yake kwa kujumuisha maeneo makuu manane ambayo yamelengwa kufikiwa ifikapo mwaka 2015.

8. MAENDELEO KATIKA BAADHI YA SEKTA ZA UCHUMI

Kilimo

Katika kipindi cha miaka minne, sekta ya kilimo imekua kwa wastani wa asilimia 4.5 kwa mwaka. Mwaka 2005, sekta ilikuwa na ukuaji wa asilimia 6.1 ukuaji ambao ni wa juu katika kipindi cha miaka minne iliyopita. Hata hivyo, hadi kufikia mwaka 2008, ukuaji wa sekta ulikuwa asilimia 4.5. Ukuaji huu umesababishwa hali ya hewa isiyotabirika na kupelekea mvua kukosekana katika baadhi ya maeneo nchini. Pamoja na kasi ya ukuaji wa sekta kupungua kumekuwapo na mafanikio katika upande wa umwagiliaji. Katika mwaka 2005 eneo lililomwagiliwa liliongezeka kutoka hekta 264,388 mwaka 2005 hadi hekta 289,245 mwaka 2008. Ongezeko hilo limetokana na ujenzi wa mabanio ya skimu za maji; matumizi ya teknolojia za umwagiliaji kwenye kanda mbalimbali.

Pamoja na ukuaji katika sekta hii, bado kuna changamoto zinazoikabili sekta hii hasa upungufu wa mvua katika baadhi ya maeneo ya nchi na hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara na upatikanaji wa malisho ya mifugo. Katika kipindi hicho mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa ambao ulikuwa ni asilimia 26.1 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 24.0 mwaka 2008. Kupungua kwa mchango wa sekta hii kunatokana na maendeleo katika sekta nyinginezo kukua kwa kasi zaidi.

Viwanda

Katika miaka minne iliyopita Serikali iliendelea na jitihada za kuimarisha maendeleo ya Viwanda Vidogo na vya Kati (SME) na kuongeza thamani ya bidhaa zinazalishwa kwa kusindika bidhaa za kilimo; kuvutia Uwekezaji katika sekta za uzalishaji, kuongeza upatikanaji wa soko na kuboresha teknolojia, kuimarisha Taasisi za Maendeleo zinazojihusisha na Utafiti; na kutoa mafunzo ya ujasiriamali.

Shughuli za viwanda zilikua kwa wastani wa asilimia 9.5 kwa mwaka katika kipindi cha miaka minne iliyopita. Ukuaji wa shughuli za uzalishaji zilikua hasa kutokana na kuimarika kwa uzalishaji wa umeme, kuendelea kuimarika kwa uzalishaji katika viwanda vilivyobinafsishwa pamoja na maendeleo ya maeneo maalum ya uwekezaji (Special Economic Zones - SEZs) chini ya *the Mini Tiger Plan*. Aidha, sera za Serikali katika kukuza biashara ndogo ndogo na za kati, pamoja na sera za kuvutia za biashara na kodi, zimechangia kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji.

(i) Mwaka 2005 sekta ya Viwanda iliweza kukua kwa asilimia 9.6 ikilinganishwa na asilimia 9.9 mwaka 2008. Ukuaji huu ulitokana hasa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa kama vile saruji, vinywaji, mabati, nondo, vyombo/vifaa vya plastiki na nguo, na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa zilizouzwa nje. Mchango uzalishaji viwandani katika Pato la Taifa uliongezeka hadi asilimia 9.4 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 8.9 mwaka 2005.

(ii) Katika mwaka 2008, ukuzaji rasilimali uliongezeka kufikia shilingi bilioni 7,381.3 kutoka shilingi bilioni 6,209.7 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 18.9.

Kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA), Serikali iliweka kipaumbele katika kurekebisha mfumo wa sera, sheria na taratibu katika maeneo ambayo mazingira wezeshaji yanatoa nafasi ya pekee ya kuchangia maendeleo ya sekta binafsi. Ili kupunguza urasimu wa kufanya biashara nchini, Serikali inatekeleza Sheria ya Uandikishaji wa Shughuli za Biashara (BARA) ya mwaka 2007.

Madini

Katika kipindi cha miaka minne sekta ya madini imekua kwa wastani wa asilimia 11.2 kwa mwaka. Kwa ujumla sekta ya madini imekuwa na ukuaji vizuri katika miaka miwili ya mwanzo (2005-2007), ingawa kufuatia msukosuko wa uchumi wa dunia sekta ya madini iliathiriwa kutokana na kupungua kwa mitaji ya wawekezaji katika sekta hiyo. katika mwaka 2005, sekta ya madini ilikua kwa asilimia 15.7 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.5 mwaka 2008. Pamoja na ukuaji wa sekta hii kupungua bado sekta hii ndio inayoongoza katika mauzo ya bidhaa nje.

Nishati

Nishati ni nyenzo muhimu katika kukuza uchumi na kupambana na umasikini. Hata hivyo takwimu zinaonyesha kuwa Watanzania wapatao asilimia 90 wanategemea nishati itokanayo na mazao ya misitu kama vile kuni na mkaa, nishati hii huchangia katika uharibifu wa mazingira. Serikali iliendelea kuhamasisha uendelezaji wa matumizi ya nishati mbadala na jadidifu. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji na usambazaji wa teknolojia muafaka ili ziweze kutumika kuleta maendeleo kwa wananchi

Katika kipindi cha miaka minne sekta ya nishati hasa umeme ilikumbwa na matatizo makubwa yakiwemo yale ya athari za kupanda kwa bei na upungufu wa kina cha maji katika kufua umeme. Katika mwaka 2006, sekta ya Nishati iliathirika sana na hali ya ukame uliyoikumba nchi na kupanda kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia katika mwaka 2006, ambapo kwa pamoja vilisababisha upungufu mkubwa wa uzalishaji umeme unaotokana na nguvu za maji na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji wa umeme unaotumia mafuta. Kiwango cha ukuaji wa umeme katika mwaka 2005 kilikuwa asilimia 9.4 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2008.

Ujenzi

Shughuli za kiuchumi katika ujenzi zilikua kwa wastani wa asilimia 9.8 kwa mwaka. Katika mwaka 2005, sekta ya ujenzi ilikua kwa asilimia 10.1 na kuongezeka hadi kufika asilimia 10.4 mwaka 2008. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi wa: barabara na madaraja; majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi; na uendelezaji wa ardhi. Mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 6.2 mwaka 2005 na kuongezeka hadi asilimia 6.7 mwaka 2008.

Katika kipindi hicho cha miaka minne iliyopita, mkazo uliwekwa katika shughuli za ujenzi ni pamoja na kuwa na mtandao wa barabara zinazopitika katika kipindi chote cha mwaka kwa kuhakikisha kuwa mikataba yote ya miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara inayoendelea inakamilishwa kwa wakati na ubora unaotakiwa. Choro hapo chini unaonesha mwenendo wa sekta kuu za kiuchumi kutoka mwaka 2004 hadi 2008. Mchoro hapo chini unaonesha mwenendo wa baadhi ya sekta.



HUDUMA ZA JAMII

Elimu

Kiwango cha ukuaji katika shughuli za utoaji huduma za elimu kilikuwa na wastani wa asilimia 5.4 kwa mwaka. Ukuaji wa hudumza za elimu umeongezeka kutoka asilimia 4.0 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 6.9 mwaka 2008. Ukuaji katika shughuli za utoaji huduma za elimu ulitokana hasa na kuendelea kwa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Elimu za Msingi na Sekondari (MMEM na MMES); na kuongezeka kwa ajira mpya za walimu. Katika kutekeleza Mipango hii mafanikio yamepatikana katika maeneo ya:

(i) Kuongeza ujuzi na idadi ya walimu na wakufunzi, kwa kutoa mafunzo zaidi kwa walio kwenye ajira na kuajiri wapya, ili kuboresha uwiano wa mwalimu na wanafunzi katika ngazi zote. Hadi kufikia mwaka 2008, uwiano wa mwalimu na mwanafunzi ulikuwa ulikuwa 1:54 ikilinganishwa na 1:58 mwaka 2004.

(ii) Kujenga nyumba za walimu, hususan kwenye maeneo yaliyo katika mazingira magumu; na

(iii) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika ngazi zote.

Afya

Kiwango cha ukuaji katika shughuli za utoaji huduma za afya kilikuwa asilimia 8.1 mwaka 2005, ikilinganishwa na asilimia 9.0 mwaka 2008. Ukuaji ulichangiwa hasa na utekelezaji wa programu za chanjo, malaria, kifua kikuu na VVU/UKIMWI. Badhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

i. Kuongezeka kwa vyombo vya kutolea tiba kutoka vituo 5180 mwaka 2005 hadi vituo 5422;
ii. Kupungua kwa vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka 111 kwa kila watoto 1000 hadi 91 kwa kila watoto 1000;
iii. Idadi ya wajawazito wanaopata madawa ya kurefusha maisha (ARV) imeongezeka kutoka wajawazito 713,509 mwaka 2007 hadi 958,103 mwaka 2008;
iv. Vituo vya ushauri vimeongezeka kutoka 515 mwaka 2005 hadi 1,743 mwaka 2008;
v. Mafanikio katika kutibu kifua kikua yamefika asilimia 86 lengo la WHO ni asilimia 86; na
vi. Maambukizi ya VVU yamepungua hadi asilimia 2.4 mwaka 2008 kutoka asilimia 3.5 mwaka 2004 kwa vijana wenye umri wa miaka kati ya 15 na 24.

Maji

Upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini umeongezeka kwa kiwango kikubwa kutoka mwaka 2005 hadi mwaka 2008. Sekta ya maji katika kipindi cha miaka minne imekua kutoka asilimia 4.5 mwaka 2005 hadi asilimia 6.6 mwaka 2008. Kukua kwa sekta hii kumetokana na utekelezaji wa miradi ya maji katika miji na vijiji kama mradi wa maji wa Shinyanga – Kahama na ule wa jiji la Dar es salaam. Upatikanaji wa maji mijiji umeongezeka hadi kufikia mita za ujazo 202.34 milioni mwaka 2008/09, na usambazaji maji umeongezeka hadi kufikia asilimia 84 mwaka 2008/09 kutoka asilimia 79.9 mwaka 2007/08. Kwa upande wa upatikanaji maji vijijini kumekuwepo na ongezeko kutoka asilimia 57.1 mwaka 2007 hadi asilimia 60.1 mwaka 2009.

9. TATHMINI YA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2025

Ni miaka kumi imepita tangu kuanza rasmi utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mafanikio yameanza kuonekana katika baadhi ya maeneo pamoja na kwamba kumekuwepo na changamoto nyingi katika kufikia malengo

ya muda mrefu ya maendeleo ya nchi. Kwa upande wa malengo ya uchumi jumla, Pato la Taifa lilitarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 8-9 kati ya mwaka 2005 – 2010 kutoka wastani wa asilimia 4 mwaka 2000. Pamoja na kuwa wastani wa ukuaji wa uchumi kwa sasa ni asilimia 7.4 mwaka 2008, kiwango ambacho kama uchumi wetu haungekumbwa na athari za msukosuko tungalifikia angalau asilimia 8. Hata hivyo, kutokana na athari za msukosuko, matarajio ni kuwa na ukuaji wa asilimia 6.2 mwaka 2010, bado viwango hivi havijafikia makadirio ya malengo katika Dira. Ukiondoa athari za msukosuko bado kuna changamoto za kimuundo katika uchumi (Structural Bottlenecks) wetu kwa mfano, kuwepo kwa ukame kwa miaka ya hivi karibu ambako kumesababisha uchumi kutotengamaa kama matarajio ya Dira 2025.

Kwa upande wa hali bora ya maisha, ingawa kuna baadhi ya malengo yaliyowekwa bado hayajaleta matunda yaliyotarajiwa ipasavyo, lakini yapo baadhi ya maeneo ambayo tayari vigezo vinaashiria kuwepo kwa mwenendo mzuri wa kufikia malengo ya 2025. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na yale ya uandikishwaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule, kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na sekondari kwa kuzingatia jinsia, kupungua kwa vifo vya watoto wachanga, kuwa na akiba ya chakula (Food Sufficiency Ratio) kwa asilimia 100 ingawa hifadhi ya chakula ambayo inahitajika angala kuwa na chakula cha miezi minne inakumbwa na matatizo ya kubadilika kwa hali ya hewa, upatikanaji wa maji ndani ya muda wa dakika 30 umeboreka kutoka asilimia 42 mwaka 2002 hadi asilimia 54 mwaka 2005. Katika upande wa jinsia dalili nzuri zimeanza kuonekana hasa uwiano wa watoto kwa jinsia wanaojuinga na shule za msingi na sekondari. Aidha katika ngazi ya Serikali hasa uongozi katika vijiji na bunge kumekuwa na mafanikio ya kuridhisha.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 bado ni muhimu kwa maendeleo ya Tanzania kwa sababu ni kitu pekee ambacho kinatoa mwelekeo wa kufikia malengo ya muda mrefu ya nchi. Kinachohitajika ni kujipanga kwa ajili ya kutekeleza kipindi kilichosalia.

10. MAPATO YA NDANI

Katika kipindi cha miaka minne, Wizara ya Fedha na Uchumi, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imefanya marekebisho ya mifumo na viwango vya baadhi ya kodi. Hatua hii imesaidia kuweka mazingira mazuri zaidi ya uzalishaji kurahisisha ukusanyaji wa kodi. Aidha, wigo wa kodi umeongezeka katika kipindi hicho. Vyanzo vipya vya mapato ya kodi ambavyo Mamlaka ya Mapato imeanza kukusanya katika mwaka wa fedha 2009/10 ni pamoja na kutoza VAT kwenye huduma za upangishaji na ukodishaji wa nyumba na majengo (Leased Buildings

and Serviced Apartments) isipokuwa zile zinazotolewa na Shirika la Nyumba la Taifa.

Kufuatia maboresho katika mfumo mzima wa ukusanyaji kodi, mapato ya ndani ya Serikali yameongezeka kwa asilimia 149 kutoka shilingi bilioni 1,951.3 mwaka 2005/06 hadi shilingi bilioni 4,855,934 mwaka 2009/10. Makusanyo ya Kodi yamefikia zaidi ya wastani wa shilingi bilioni 400 kwa mwezi ikilinganishwa na bilioni 150 kwa mwezi mwaka 2005/06. Jedwali hapo chini linaonesha mwenendo wa Mapato katika kipindi cha miaka minne iliyopita.

Mwenendo wa Mapato ya Ndani Serikali 2004/05 hadi 2009/10 (Tsh Milioni)

	2005/06 Halisi	2006/07 Halisi	2007/08 Halisi	2008/09 Halisi	2009/10 Bajeti
Jumla ya Mapato	**2,124,843.70**	**2,739,022.40**	**3,634,580.60**	**4,284,779.70**	**5,096,016.10**
A. Mapato ya Kodi	1,946,432.60	2,529,439.40	3,359,249.80	4,044,717.10	4,855,934.90
1.Ushuru wa Forodha	190,855.80	242,831.80	289,275.60	359,255.30	448,174.40
2.Ushuru wa Bidhaa	261,550.30	520,078.10	660.888.2	762,026.20	993,790.70
3.Kodi ya VAT	803,024.60	831,627.90	1,042,489.70	1,231,201.80	1,400,189.10
4.Kodi ya Mapato	554,048.00	716,320.50	983,804.30	1,228,642.40	1,498,712.60
5.Kodi Nyingine	136,954.00	218,581.10	382,792.00	463,591.30	515,068.10
B:Mapato yasiyotokana na Kodi	**178,411.10**	**209,583.00**	**275,330.80**	**195,062.60**	240,081.20
1.Gawio la Mashirika	13,232.20	10,567.50	58,253.50	25,865.90	25,597.00
2.Wizara Nyingine na Mikoa	124,642.20	131,080.10	172,797.30	155,334.50	12,777.50
3.Mapato mengine yasiyo ya Kodi	40,536.70	67,935.40	44,280.00	44,247.30	201,706.70

Chanzo: Wizara ya Fedha na Uchumi

11. MAPATO YA KODI

Mapato ya Serikali hujumuisha mapato yatokanayo na Kodi na mapato yasiyo ya Kodi. Ili kuongeza mapato yake, Serikali hufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbali mbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi. Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza wigo wa kodi na hatimaye kukusanya mapato zaidi ili kugharamia matumizi yake. Kwakuwa mapato haya hayatoshelezi matumizi ya Serikali, Serikali hulazimika kutafuta mapato ya ziada kutoka Fedha za nje ikiwa ni pamoja na kupata misaada na mikopo kutoka kwenye vyombo vya kimataifa na nchi aahisani.

MWENENDO WA MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI

Mafanikio ya Usimamizi wa kodi yameiwezesha Serikali ya Awamu ya Nne kukuza makusanyo mapato yote kutoka Sh. 2,167.6 bilioni mwaka 2005/06 hadi kufikia kiwango cha juu cha makusanyo cha Sh. 5,096,016.8 bilioni mwaka 2009/10. Mwenendo wa wastani wa makusanyo ya mapato ya ndani kwa mwezi kwa

kipindi kati ya mwaka 2005/06 hadi 2009/10 umeoneshwa katika jedwali hapa chini.

Wastani wa Makusanyo ya Mapato kwa Mwezi										
	2005/06		2006/07		2007/08		2008/09		2009/10	
	lengo	halisi	lengo	halisi	lengo	halisi	lengo	halisi	lengo	halisi
Makusanyo kwa mwezi	173,097.6	180,633.9	205,082.9	230,664.3	293,131.9	303,750.5	399,135.0	357,065.0	437,422.4	-

Chanzo: Wizara ya Fedha na Uchumi

MAPITIO YA MAKUSANYO YA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI HADI NOVEMBA 2009

Mapato ya kodi katika kipindi cha Julai- Novemba 2009 yalikuwa Tsh. 1,737.2 billioni ikilinganishwa na lengo la Tsh 1,923.4 billioni. Kiwango hiki ni sawa na asilimia 90 ya lengo. Mapato yasiyo ya kodi kwa kipindi hicho yalikuwa Tshs. 87.9 billioni ikilinganishwa na lengo la Tshs. 103.3 billioni kiasi hicho cha makusanyo ni sawa na asilimia 85 ya lengo. Viwango vidogo vya makusanyo katika kipindi hicho cha (July – Novemba 2009) vimechangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo mtikisiko wa hali ya uchumi duniani.

MATARAJIO YA MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI KWA MWAKA 2009/10

Sera za mapato mwaka 2009/10 zinalenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua Shilingi milioni 5,096,016 sawa na 16.4% ya Pato la Taifa. Kati ya hayo,

i. Mapato ya Kodi ni Shilingi 4,855,935 milioni.
ii. Mapato yasiyo ya Kodi Shilingi 240,081 milioni.
iii. Mapato ya Ubinafsishaji ya Shilingi 15,000 milioni.
iv. Mapato ya Halimashauri ya Shilingi 138,052 milioni.
v. Mikopo ya Ndani Shilingi 1,082,669 milioni.
vi. Mikopo na Misaada ya Nje, ikijumuisha MDRI na MCA (T), ni Shilingi milioni 3,181,947.

Jumla ya mapato yamekadiriwa kuwa Shilingi milioni 9,513,685, ambayo yatatumika kugharamia matumizi ya kiwango hicho.

HATUA ZA KUIMARISHA UKUSANYAJI MAPATO:

Serikali imekuwa ikichukua hatua za kuongeza mapato kwa kufanya marekebisho ya sera za kodi na kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa nia ya kupanua wigo wa mapato bila kuathiri ukuaji wa Uchumi. Aidha sera za mapato pamoja na kuzingatia azma ya kuongeza mapato ya ndani zinazingatia kutoa vivutio vyenye kuwezesha kukua kwa uchumi katika muda wa kati na mrefu.

Baadhi ya hatua ambazo Serikali imechukua hivi karibuni ni pamoja na:-

(i) Kupunguza kiwango cha kodi ya Ongezeko la Thamani kutoka asilimia 20 ya mauzo hadi asilimia 18 ya mauzo. Punguzo hili linakusudiwa kuongeza kiwango cha ulipaji kodi kwa kiasi.

(ii) Kufuta misamaha ya kodi iliyokuwa imetolewa kwenye matangazo ya Serikali 405 yaliyokuwa yametolewa kati ya mwaka 1964 na 2005. Aidha matangazo hayo yalikuwa yametolewa bila kuwa na ukomo wa kutumika au kuainisha wazi kodi zinazosamehewa.

(iii) Kuondoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petroli uliokuwa unatolewa kwa makampuni ya madini kupitia tangazo Namba 480 la mwaka 2002.

(iv) Kusamehe ushuru wa forodha kwenye vipuri vya viwanda, kwa kufuata utaratibu na vigezo maalum. Lengo lilikuwa kupunguza gharama za uzalishaji viwandani.

(v) Katika kipindi cha mwaka mmoja ushuru wa forodha kwa magari yenye tani 5 umepunguzwa toka asilimia 25 hadi asilimia 10 ambapo ushuru umeondolewa kwa yenye tani zaidi ya 20. Hatua hii imelenga kupunguza gharama za usafirishaji na kuhamasisha uzalishaji.

Pamoja na kuongezeka kwa makusanyo ya kodi, bado changamoto mbalimbali zimeikabili Wizara na hivyo kutoweza kuvuka malengo yake iliyojiwekea.

MIKAKATI YA KUONGEZA MAPATO

(i) Kupanua Wigo wa Kodi

Mikakati ya Wizara imeelekezwa katika maeneo yafuatayo:-

- Kuboresha utaratibu wa kusimamia Kodi kwa msingi wa **Vitalu vya Walipa Kodi (Block Management System)** na kuangalia uwezekano wa kutumia Utaratibu wa Taarifa ya Jiografia za Maeneo (Geographical Information System).

- Kuhakikisha kuwa walipa Kodi wote wanalipa Kodi yao halali na kuwa wanaandikishwa kama walipa Kodi kwenye hifadhi kuu ya taarifa ya walipa Kodi (taxpayers' data base) inayotunzwa na TRA.
- Kuendelea kuboresha utendaji wa Idara ya Walipa Kodi Wakubwa kwa kuipa uwezo zaidi wa kukagua biashara (Tax audit) za walipa Kodi wake.
- Kuendelea na juhudi za kuingiza kwenye wigo wa Kodi shughuli zilizoko kwenye sekta isiyo rasmi kwa kushirikiana na mipango husika kama:
    a. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA),
    b. Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBITA) pamoja na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa shughuli za Sekta isiyo rasmi zinachangia katika mfuko wa mapato ya taifa,

(ii) Kuimairisha Ulipaji Kodi kwa Hiari (Compliance) na Kusimamia Sheria za Kodi (Enforcement)

- Kushirikiana na wadau wetu wakiwemo washauri wa mambo ya Kodi ili kuboresha uwajibikaji.
- Kufanya utafiti wa mara kwa mara wa kujaribu kuangalia kiwango cha mwitikio (compliance level) wa kulipa Kodi kulingana na uzio uliopo kwa lengo la kuainisha vianzo vya uvujaji mapato na kuimarisha usimamiaji wa sheria.
- Kuendelea kutumia mfumo wa kulipa Kodi kwa kuzingatia viashiria mbalimbali vya hatari ya kupoteza mapato ya Serikali **(risk management techniques)** ili kuzuia uwezekano wa upotevu wa mapato ya Serikali.
- Kuboresha mfumo wa kufuatilia mwelekeo wa mizigo ya mafuta ya petroli na mizigo mingine yenye kiwango kikubwa cha viashiria vya hatari.
- Kuimarisha matumizi ya mitandao ya kompyuta (electronic systems) ili kupunguza muda wa huduma na hivyo kuwapunguzia walipa Kodi gharama za kulipa Kodi.
- Kuimarisha utaratibu wa kukagua bidhaa baada ya kutoka bandarini **(post clearance audit).**

(iii) Kuboresha Mifumo ya Utendaji.

- Kuongeza ufanisi katika utumiaji wa mfumo wa utawala bora **(Quality Management Systems "QMS 9001:2000")** kwa Mamlaka;
- Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu matumizi ya teknolojia katika kukusanya Kodi.
- Kuboresha zaidi matumizi ya Mtandao wa kompyuta wa **ASYCUDA++** ili uweze kutumika kwa **Tovuti (internet)**.

- ❖ Kuandaa utaratibu wa kufungamanisha (integration of the systems) michakato ya **ASYCUDAA++** na Forodha na hatimaye kuondokana na utaratibu wa kutumia huduma za **TISCAN**.
- ❖ Kukamilisha uundaji wa mfumo wa kutunza taarifa za Kodi wa *Integrated Tax System* (**ITAX)**.
- ❖ Kuboresha mfumo wa marejesho ya Kodi **(Tax Refund System)**.

(iv) Kupambana na ukwepaji Kodi

- ❖ Kuendeleza ushirikiano na mamlaka nyingine za mapato za: Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki (EAC-CU), Umoja wa Maendeleo wa Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC); na nchi nyinginezo katika kubadilishana uzoefu na kupashana habari (Information Exchange).
- ❖ Kuoanisha mifumo ya Kodi zetu na nchi tunazoshirikiana kiuchumi ili kuondoa vikwazo na tofauti zinazoweza kuwa kivutio cha ukwepaji Kodi.
- ❖ Kuendelea kuboresha programu za ukaguzi hasa kwa Kodi ambazo ukusanyaji wake unaenda kwa misingi ya ukaguzi, kama vile *Kodi ya Makampuni, Kodi ya Mapato ya Biashara (Presumptive tax),* na *Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).*
- ❖ Kuimarisha usimamizi wa bidhaa zinazopitia hapa nchini kwa ajili ya matumizi ya nchi jirani (transit cargo): Hasa bidhaa za petroli kupitia uandikishwaji wa Kampuni husika za kuingiza mafuta ya petroli kwenye nchi mafuta yanakokwenda.
- ❖ kufanya ukaguzi wa pamoja na vyombo vya nchi husika kwa bidhaa zinazopitia hapa nchini na
- ❖ kuhakikisha kuwa nyaraka zote za kutoa mizigo ni sahihi; na
- ❖ Kuimarisha usimamiaji wa misamaha ya Kodi ili kuzuia mianya ya matumizi mabaya ya misamaha hiyo kwa malengo ya kukwepa Kodi.

CHANGAMOTO

i. Kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuboresha upatikanaji wa takwimu za mapato ya Serikali yanayokusanywa na Wizara, Idara na Taasisi nk.
ii. Asasi na Wakala mbalimbali wanaotoza Kodi ya huduma kuchangia sehemu ya mapato mfuko mkuu wa Serikali.
iii. Kubuni mfumo bora wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya Kodi na utoaji wa taarifa za makusanyo.
iv. Kuboresha na kuimarisha utekelezaji wa sera na sheria zinazosimamia mapato.
v. Kukua kwa Sekta isiyo rasmi ni changamoto ambayo inahitaji kufanyiwa kazi ili iweze kuingizwa kwenye wigo wa mapato.
vi. Kudhibiti ukwepaji Kodi na hasa ushuru wa mafuta kwa mafuta yanayoingizwa nchini hasa:-

a. Uchanganyaji wa mafuta ya diseli na mafuta ya taa.
b. Mafuta yanayosafirishwa nje yamekuwa yakiuzwa hapa nchini na hivyo kukwepa kulipa ushuru wa mafuta.

12. MWENENDO WA DENI LA TAIFA

Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Madeni ili kuthibiti ongezeko la Deni la Taifa lisizidi kiwango kinachohimilika.

Deni la Taifa

Wizara imeendelea kutekeleza Sera na Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Madeni ili kuthibiti ongezeko la Deni la Taifa lisizidi kiwango kinachohimilika.

Hadi Juni 2009, deni la Taifa lilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 8.25, kati ya hizo Dola za Kimarekani bilioni 5.69 ni deni la nje na Dola za Kimarekani bilioni 2.60 ni deni la ndani. Deni la Taifa liliongezeka katika kipindi cha mwaka 2000/01 na 2005/06 na kupungua kwa kiasi kikubwa mwaka 2006/07 hadi kufikia Dola za Kimarekani bilioni 7.53 kutoka Dola za Kimarekani bilioni 10.01 mwaka 2005/06. Mikopo mipya kutoka ndani na mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje, kushuka kwa thamani ya shilingi na malimbikizo ya riba hasa kutoka katika nchi zisizo wanachama wa Paris Club na mikopo ya kibiashara ndio iliyosababisha kuongezeka kwa deni la Taifa. Aidha, Tanzania ilieendelea kupata misamaha mbalimbali ya madeni kutoka nchi wahisani na mashirika mbalimbali chini ya utaratibu wa (HIPC na MDRI) na hivyo kupunguza deni la Taifa kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.



Chanzo: 2008 'Debt sustainability Analysis Report'

Mwenendo wa Viwango vya Deni kuwa Himilivu (Performance of Key debt indicators)

Kwa mujibu wa mwenendo wa viwango vya deni kuwa himilivu, deni la Taifa linaonyesha kuwa linadhibitiwa na linahimilika. Aidha, uwiano wa deni kwa Pato la Taifa umeendelea kupungua kutoka asilimia 65.6 mwaka 2000/01 hadi kufikia asilimia 30.2 mwaka 2007/08. Katika mwaka 2000/01, uwiano wa deni la nje kwa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 55.3, kiwango hicho kilipungua zaidi hadi kufikia aslilmia 36.3 mwaka 2005/06 na mwaka 2007/08 kiwango hiki kilifikia asilimia 16.6. Jedwali hapa chini linaonesha mwenendo wa viwango vya deni la Taifa.

Kigezo	2000/01	2001/02	2002/03	2003/04	2004/05	2005/06	2006/07	2007/08
% Deni la Serikali / Pato la Taifa	65.6	61.6	58.4	53.5	48.9	50.8	48.2	30.2
% Deni la nje/Pato la Taifa	55.3	51.5	47.7	43	37.6	36.3	31.6	16.6
%Deni la ndani/Pato la Taifa	10.3	10.1	10.7	10.5	11.3	14.5	16.6	13.6
%Ulipaji wa Deni/Mapato	18.2	14.6	11.5	11.9	10.2	9.2	3.1	1.5

Chanzo: 2008 'Debt sustainability Analysis Report'

Mikopo na Misaada

Nchi yetu imeendelea kupokea mikopo na misaada kupitia misaada ya kibajeti (General Budget Support) na kutoka katika miradi. Katika mwaka 2008/09, Serikali ilipokea misaada na mikopo yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni

1.7. Kati ya fedha hizo, Dola za Kimarekani milioni 726.5 zilikuwa mkopo na Dola za Kimarekani milioni 967.6 zilikuwa msaada. Aidha katika mwaka 2005/06, Serikali ilipokea misaada na mikopo yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni moja kati ya fedha hizo, Dola za Kimarekani milioni 651 zilikuwa mkopo na Dola milioni 349 zilikuwa msaada.

13. USIMAMIZI WA MATUMIZI

Usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali ni moja ya jukumu muhimu la Wizara ya Fedha na Uchumi. Usimamizi huu unalenga kupata thamani halisi ya fedha za Serikali na kuhakikisha fedha hizo zinatumika katika maeneo yaliyokusudiwa. Mafanikio yamepatikana katika kuimarisha usimamizi wa fedha za umma.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikani ni yafuatayo:

i. Kuongeza idadi ya wahasibu na wakaguzi katika ngazi zote. Tayari wizara imeajiri wahasibu na wakaguzi katika ngazi za Wizara, Idara na serikali za mitaa ili kudhibiti matumizi ya umma;
ii. Kuanzishwa kwa kitengo cha ufuatiliaji wa matumizi ya umma (bajeti) katika miradi iliyoidhinishwa kwenye bajeti (Expenditure Trucking Unit);
iii. Ofisi ya Mkaguzi Mkuu (CAG) imeongezewa nguvu za kisheria kuweza kufanya kazi zake bila kuingiliwa na taasisi yoyote;
iv. Jitihada zimefanyika ili kuhakikisha kuwa CAG ina ofisi katika kila wilaya nchini ili kuweza kutimiza majukumu yake kwa ufanisi zaidi;
v. Sheria ya manunuzi ya umma inaendelea kufanyiwa marekebisho ili kuondoa mapungufu yaliyopo;
vi. Kutoa mafunzo kwa wizara na idara mablimbali juu ya matumizi ya sheria ya manunuzi ya umma kutokana na malalamiko kuwa baadhi ya watendaji wanashindwa kuitumia sheria hiyo ipasavyo;
vii. Kuangalia upya utaratibu wa kutumia sheria ya manunuzi wakati wa kuwa na matumizi ya dharura;
viii. Kupunguza muda katika utumiaji wa sheria ya manunuzi;
ix. Kushirikiana na kamati za bunge za hesabu za serikali kuu na zile za serikali za mitaa na mashirika ya umma katika kusimamia matumizi ya umma;
x. Mchakato unaendelea katika kuanzisha ofisi ya naibu mhasibu mkuu katika ngazi ya serikali za mitaa; na
xi. Mchakato umeanza wa kuanzisha idara ya ukaguzi wa ndani ili kuweza kuhakiki hesabu za wizara na taasisisi kabla ya ukaguzi wa nje.

14. KUZIPATIA RASILIMALI FEDHA SEKTA MBALI MBALI

Wizara imeendelea kutoa rasilimali fedha kwa sekta mbalimbali ili kuweza kutekeleza majukumu yao. Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Nne, Wizara ya Fedha na Uchumi imeelekeza rasilimali fedha kwa kiwango kikubwa katika maeneo hayo. Wizara ya Fedha na Uchumi imetenga fedha nyingi zaidi katika kuboresha huduma za jamii hususan Elimu pamoja na Afya. Mgawanyo wa rasilimali fedha katika maeneo ya kilimo, miundombinu, elimu na afya kwa kipindi cha miaka minne (2006/7 – 2009/10) ni kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali hapo chini.

Fedha zilizotengwa kwenye maeneo ya kipaumbele (shilingi bilioni)

No	Sekta	Mgao				
		2006/07	**2007/08**	**2008/09**	**2009/10**	**Jumla**
1	Kilimo	315.32	379.00	513.00	666.90	**1,874.22**
2	Miundombinu	611.23	777.20	973.30	1,096.60	**3,458.33**
3	Afya	456.96	589.90	910.80	963.00	**2,920.66**
4	Elimu	873.18	1,086.10	1,430.90	1,743.90	**5,133.58**



Chanzo: Bajeti ya Serikali

Kwa kutambua umuhimu wa sekta hizi katika kuimarisha uchumi na ustawi wa jamii, Wizara ya Fedha na Uchumi imekuwa ikitenga wastani wa kiasi cha asilimia 50 ya bajeti yote ya mwaka kutekeleza miradi mbalimbali katika sekta za Elimu, Kilimo, Miundombinu na Afya kwa kipindi cha kuanzia 2006/7 hadi 2009/10.

15. SEKTA ZA KIJAMII

Katika mwaka 2009/10 Serikali imetenga kiasi kikubwa cha fedha kwa sekta muhimu pamoja na maeneo yenye mazingira magumu ukilinganisha na mwaka 2005/06 kama ifuatavyo:-

(i) Sekta ya afya imetengewa shilingi bilioni 963.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 365.8 mwaka 2005/06;

(ii) Sekta ya elimu imetengewa shilingi bilioni 1,743.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 669.5 mwaka 2005/06;

(iii) Sekta ya maji imetengewa shilingi bilioni 347.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 159.9 mwaka 2005/06; na

(iv) Jumla ya Shilingi milioni 22,650 zimetengwa ili kugharamia miradi maalum katika maeneo yenye mazingira magumu yasiyovutia watumishi kufanya kazi.

16. USIMAMIZI WA SEKTA YA FEDHA

Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kufanya mageuzi katika Sekta ya Fedha ambayo yanalenga zaidi kurekebisha Sera na Sheria mbalimbali za fedha ili kuongeza uwazi na ushindani katika utoaji wa huduma za kibenki na hivyo kurahisisha upatikanaji wa mikopo ikiwa ni pamoja na kupunguza riba kwa wakopaji.

17. KUWEZESHA UPATIKANAJI WA MIKOPO

Mikopo iliyotolewa na mabenki kwa sekta binafsi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi iliongezeka kutoka shilingi bilioni 1,571.0 mwezi Desemba 2005 hadi shilingi bilioni 4,710.2 mwezi Juni 2009, sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 34.5 kwa mwaka. Mwezi Oktoba 2009 mikopo hiyo ilikuwa imefikia shilingi bilioni 4,836.0. Aidha, wastani wa riba kwa dhamana zote ilishuka kutoka asilimia 16.4, mwezi Septemba 2007 hadi asilimia 7.0 mwezi Aprili 2008. Mwezi Februari 2009 riba ilipanda na kufikia asilimia 13.3 na kushuka hadi asilimia 5.2 mwezi Oktoba 2009.

18. KUWAWEZESHA WAJASIRIAMALI

18.1 Mifuko ya Dhamana ya Mikopo (Credit Guarantee Scheme)

Kuanzishwa kwa Mfuko wa Dhamana wa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati (SME Credit Guarantee Scheme) ambao unaratibiwa na Benki Kuu

kumeboresha mazingira ya wenye mitaji midogo na ya kati waweze kupata mikopo kutoka kwenye mabenki na taasisi za fedha. Tangu mfuko huu uanzishwe, jumla ya SMEs 48 zimepata udhamini wa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.054. Kati ya wajasiliamali hao, sekta ya uzalishiji inaongoza ikifuatiwa na sekta za ujenzi na kilimo. Ili kuleta ufanisi zaidi, mwaka huu Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 10 kuongeza mtaji wa mfuko wa wajasiliamali wadogo na wa kati.

18.2 Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi wa wajasiriamali wadogo (Mfuko wa JK)

- Kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi kwa ajili ya wajasiriamali wadogo kumesaidia vikundi mbalimbali kupata mikopo nafuu.

- Katika awamu ya kwanza, Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi wa JK- ilitoa kiasi cha Shilingi bilioni 10.5 kupitia benki ya NMB (Shilingi bilioni 5.25) na CRDB (Shilingi bilioni 5.25). Kiasi hiki kiliwezesha kutolewa kwa mikopo ya Shilingi bilioni 37.17 ikiwa in asilimia 118 ya Shilingi 31.5 zilizotengwa kutolewa na benk hizo mbili. Hadi kufikia Juni 30, 2009 jumla ya wajasiliamali 44,224 walikuwa wamefaidika na mikopo iliyotolewa ikiwa na uwiano wa wanaume 30,072 na wanawake 14,152

- Katika awamu ya pili, Serikali imetoa Shilingi bilioni 10.5; kati ya hizo Shilingi milioni 600 zilipelekwa Zanzibar na Shilingi bilioni 9.9 Tanzania Bara.

- Hadi kufikia Septemba, 2009 mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 6.304 ilitolewa na benki na asasi ndogo za fedha kwa wajasiriamali wadogo.

18.3 Mfuko wa Udhamini wa mikopo kwa ajili ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi

- Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2002. Hadi June 2009 mfuko ulikuwa umetoa dhamana ya Shilingi bilioni 295.6. Kati ya dhamana hizo, kiasi cha dhamana ya shilingi bilioni 171.7 kilitolewa kati ya mwaka 2005 na 2009 pekee. Sekta nyingi zimefaidika na udhamini huu, kilimo na uzalishaji zikiongoza. Ili kuongeza ufanisi zaidi, Serikali imetenga Shilingi bilioni 10 mwaka huu ili kuongeza mtaji wa mfuko huu.

18.4 Mfuko wa kuendeleza Sekta ya maua

- Serikali ilianzisha mfuko huu ili kuendeleza sekta ya maua nchini kwa lengo la kuongeza uchumi na kuongeza ajira. Jumla ya Shilingi bilioni 50.6 zimekwisha tolewa na serikali kusaidia sekta ya maua.

18.4 Mradi wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali wadogo (SELF-PROJECT)

- Kati ya kipindi cha Desemba 2005 mpaka Desemba 2009, Mradi wa SELF ulitoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 15.8 kwa wajasiriamali wapatao 30,069 miongoni mwao asilimia 58.0 ni wanawake. Mikopo hii imewafikia walengwa kupitia Asasi za kati za fedha zipatazo 136 ambapo asilimia 81.0 ni Asasi zilizokopeshwa na Mradi zikiwa za vijijini.

- Mradi umetoa mafunzo mbalimbali kwa watendaji wapatao 938 kutoka asasi ndogo za fedha zikiwemo SACCOS 246 na NGOs 33. Vile vile jumla ya walengwa wapatao 3,472 wamepatiwa mafunzo ya jinsi ya kuendesha miradi midogo midogo kwa faida.

19. FURSA ZA AJIRA KWA VIJANA

Hali ya Ukosefu wa Ajira

Hadi kufikia mwaka 2009, na kulingana na utafiti wa ajira na nguvukazi nchini inakadiriwa kuwa nguvukazi ilikuwa na watu 20.6 milioni. Vile vile, matokeo hayo yanaonesha kuwa watu milioni 18.3 walikuwa wameajiriwa. Kati yao, watu 9.0 milioni walikuwa wanaume na wanawake 9.3 milion. Kilimo kiliendelea kuwa ajira kuu ya watu nchini.

Kwa kuzingatia tafsiri ya ukosefu wa ajira Tanzania Bara, uchambuzi wa tafiti ya mwaka 2006 unaonyesha kuwa wanaume 1.0 milioni na wanawake 1.3 milioni walikuwa hawana kazi, sawa na asilimia 11.0 ikilinganishwa na asilimia 12.9 mwaka 2000/01. Katika Jiji la Dar es Salaam, asilimia 31.4 ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi walikuwa hawana kazi ikilinganishwa na asilimia 46.0 mwaka 2000/01, miji mingine asilimia 16.3 ikilinganishwa na asilimia 26.0 mwaka 2000/01 na vijijini asilimia 7.1 ikilinganishwa na asilimia 8.0 mwaka 2000/01.

Ukosefu wa ajira kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35 umepungua kutoka asilimia 16.0 mwaka 2001 hadi kufikia asilimia 13.0 mwaka 2006. Vile vile, viwango vya ukosefu wa ajira kwa vijana wa kiume vilipungua kutoka asilimia

14.0 mwaka 2001 hadi asilimia 12.0 mwaka 2006, wakati vijana wa kike vilipungua kutoka asilimia 17.0 mwaka 2001 hadi asilimia 14.0 mwaka 2006.

Hali ya Ukosefu wa Ajira kwa Nguvukazi ya miaka 10+ kwa tafsiri mbalimbali za ajira mwaka 2001 na 2006

Kundi	DSM		Miji Mingine		Vijijini		Jumla	
	2001	2006	2001	2006	2001	2006	2001	2006
A. Anatafuta kazi (Tafsiri halisi ya Kimataifa)	20.6	16.6	4.4	3.4	0.7	0.7	2.3	2.8
B. Yupo tayari kufanya kazi lakini hatafuti kazi	5.7	4.4	5.5	2.9	2.1	0.9	2.8	1.6
A + B: Tafsiri ya Kimataifa iliyolegezwa	26.4	21.0	9.9	6.3	2.8	1.6	5.1	4.3
C. Ana ajira isiyo ya uhakika	20.1	10.3	15.9	10.0	5.6	5.5	7.8	6.3
A + B + C: Tafsiri ya Tanzania	46.5	31.3	25.9	16.3	8.4	7.1	12.9	11.0

Chanzo: Utafiti wa Nguvukazi 2006

Upatikanaji wa Ajira

Katika kipindi cha miaka minne cha Serikali ya Awamu ya Nne, mafanikio yafuatayo yamepatikana katika ajira:-

(i) Hadi kufikia Disemba, 2008, ajira mpya 1,271,923 zilitengenezwa katika sekta zifuatazo: Serikali 85,571; taasisi za Serikali 965 na sekta binafsi 1,185,387.

(ii) Mwezi Julai, 2007 Serikali iliunda Wakala wa Huduma za Ajira (Tanzania Employment Services Agency - TaESA) ili kuwaunganisha wanaotafuta kazi na waajiri.

20. KUBORESHA HUDUMA KWA WASTAAFU

- Wastaafu 53,600 ambao wapo kwenye daftari la pensheni la Hazina, wamehamishiwa katika Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) na wameanza kulipwa Pensheni zao kupitia Mfuko huo kuanzia Julai, 2008.

- Hadi kufikia Julai, 2009, idadi ya wastaafu waliokuwa kwenye orodha ya wastaafu wanaolipwa pensheni na Wizara ya Fedha na Uchumi kupitia Mfuko wa PPF, ilifikia 55,051 ikiwa ni ongezeko la wastaafu 1,451.

- Wastaafu walioko kwenye daftari la Hazina wanalipwa pensheni zao kupitia akaunti binafsi badala ya utaratibu wa kulipiwa kwenye kaunta za benki.

- Utaratibu huo umewawezesha wastaafu kupewa kadi ya huduma ya kuchukulia fedha (ATM), inayowawezesha kuchukua fedha yao wakati wowote.

- Hadi Juni, 2008, wastaafu 21,152 waliokuwa wamelipwa pensheni zao kwa mkupuo na kuondolewa kwenye daftari la wastaafu, wamerejeshwa kwenye daftari kufuatia uamuzi wa Serikali wa mwaka 2004/2005 wa kuwarejesha kwenye daftari wastaafu wote waliokuwa wamelipwa pensheni zao kwa mkupuo.

- Hadi Julai, 2009 idadi ya wastaafu waliorejeshwa kwenye daftari la wanaolipwa pensheni, iliongezeka kufikia 22,295 ikiwa ni ongezeko la wastaafu 1,143.

21. WASTAAFU WA ILIYOKUWA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

- Hadi kufikia tarehe 30/06/2009 wastaafu 31,519 wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki wamelipwa mafao yao ikiwa ni ongezeko la wastaafu 75 ikilinganishwa na wastaafu 31,444 waliokuwa wamelipwa hadi Juni, 2008.

- Kwa mujibu wa Hati ya Makubaliano, wastaafu 31,831 ndio waliotakiwa kulipwa kwa kufuata kumbukumbu za majalada yao. Hata hivyo, wastaafu 312 hawajalipwa mafao yao kwa vile kumbukumbu zinaonyesha kuwa walikuwa vibarua wakati wa Jumuiya na baadhi yao walipata ajira ya kudumu baada ya kuvunjika kwa Jumuiya na hivyo hawastahili malipo yoyote.

22. ATHARI ZA MSUKOSUKO WA UCHUMI

Tanzania iliathiriwa na awamu ya pili ya athari za msukosuko wa uchumi wa dunia. Awamu ya pili inatokana na kushuka au kuzorota kwa uchumi wa dunia. Madhara kwenye uchumi wa Tanzania yalikuwa:-

(i) Kupungua kwa bei za bidhaa muhimu ambazo Tanzania inauza nje na hivyo kupunguza mapato ya wazalishaji wa hapa nchini na pia mapato ya fedha za kigeni.

(ii) Kushuka kwa idadi na matumizi ya watalii wanaokuja Tanzania kutokana na kushuka kwa kipato cha wananchi kwenye nchi ambako watalii wengi hutokea;

(iii) Kushuka kwa kiwango cha fedha (remittances) ambazo Watanzania wanoishi katika nchi zilizoathirika zaidi hutuma kwa ndugu na jamaa zao hapa Tanzania;

(iv) Kupungua kwa mapato ya fedha za kigeni na hivyo kushuka kwa thamani ya shilingi;

(v) Kupungua kwa uwekezaji hasa wa kutoka nje (FDI), kwa sababu ya wawekezaji kushindwa kupata mitaji katika masoko ya mitaji ya kimataifa.

(vi) Kushuka kwa kiwango cha ukuaji wa uchumi;

(vii) Kupungua kwa kipato kwa ajili ya matumizi (disposable income) kwa Watanzania na hivyo kupungua kwa matumizi (consumption spending).

(viii) Kupungua kasi ya ukuaji wa mapato ya kodi na hivyo kuathiri bajeti ya Serikali katika muda wa kati.

(ix) Kuongezeka kwa kiwango cha mikopo isiyorejeshwa (default rates) katika mabenki yetu.

22.1 HATUA AMBAZO TANZANIA IMECHUKUA KUKABILIANA NA MTIKISIKO WA UCHUMI WA DUNIA

Katika jitihada za kukabiliana na athari zinazotokana na msukosuko wa kifedha na kiuchumi Duniani, Wizara ya Fedha na Uchumi ilisimamia uandaaji wa Mpango wa kuunusuru uchumi ambapo hatua za muda mfupi na muda wa kati zilipangwa kuchukuliwa. Gharama za Mpango huo wa dharura zilikadiriwa kufikia Shilingi 1.7 Trilioni zilizotokana na fedha za Serikalii na za Washirika wa maendeleo hasa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa. Hatua ambazo Serikali ilipanga kuzichukua ni pamoja na zifuatazo:

(i) kufidia hasara waliyopata wanunuzi wa mazao msimu wa 2008/09,
(ii) kutoa udhamini wa kuahirisha mikopo ya waathirika,
(iii) kutoa mitaji ya uendeshaji (working capital) kwa riba nafuu,
(iv) Kuboresha Mifuko ya Dhamana,
(v) kuhakikisha upatikanaji wa chakula,
(vi) kulinda uwekezaji muhimu hasa katika miundombinu ili kuendeleza ukuaji wa uchumi na kutekeleza malengo ya milenia, na
(vii) kutoa ruzuku kwenye bei ya mazao.

Wizara ya Fedha na Uchumi inaendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mpango huo ambapo Kufuatia juhudi hizo za Serikali waathirika wengi wameweza kufidiwa na kuwezeshwa kuendelea na shughuli zao za uzalishaji. Kwa upande wa vyama vya ushirika, navyo vimeweza kujihusisha na ununuzi wa mazao kama ilivyokusudiwa. Hali hii imewezesha wakulima kuendelea na maandalizi ya kilimo cha msimu huu wakiwa na uhakika wa pembejeo za kilimo. Taarifa ya utekelezaji wa maeneo haya hadi mwezi Septemba 2009 kwa muhtasari ni kama ifuatavyo:-

a. Kufidia hasara kwa wanunuzi – Benki Kuu ilipokea maombi 35 yenye thamani ya shilingi bilioni 28.64 kutoka kwa wanunuzi wa pamba. Tathmini ilionesha kwamba jumla ya shilingi bilioni 26.97 zilistahili kulipwa na kiasi cha shilingi bilioni 19.9 kililipwa kama fidia. Serikali inatafuta fedha zaidi kufidia waliobaki.
b. Kutoa udhamini wa kurejesha mikopo – Jumla ya shilingi bilioni 15.8 zilitolewa kama dhamana ya kurudisha mikopo. Lengo la hatua hii ni kuwawezesha wakopaji kupata mikopo mipya kwa ajili ya shughuli za ununuzi wa mazao kwa msimu wa 2009/10.
c. Kutoa ruzuku ya bei ya mazao – Kiasi cha shilingi bilioni 20.0 kilitolewa chini ya mpango huo kwa zao la pamba.
d. Kuboresha mifuko ya dhamana – Kiasi cha shilingi bilioni 12.4 kilitolewa kwa lengo la kupanua mifuko ya dhamana ya *ECGS* na *SMEs*.
e. Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 10.0 kwa ARTUMAS kama *on-lending facility* kupitia TIB; fedha hizo tayari ziko TIB.
f. Upatikanaji wa chakula – Serikali imetoa ruzuku ya pembejeo kwa wakati kwa kushirikisha mikoa yenye uwezo wa kuzalisha chakula kwa wingi, kuongeza wataalamu wa ugani na kusambaza chakula kutoka maeneo yenye ziada kwenda kwenye maeneo yenye uhaba; na
g. Uimarishaji wa Sekta ya fedha – Serikali imeendelea kusimamia na kufuatilia kwa karibu, kupitia Benki Kuu, ili kuhakikisha Sekta ya fedha haitetereki. Aidha, mabenki na taasisi nyingine za kifedha zinaendelea kuhimizwa kukopesha wazalishaji ili waongeze uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa wanazozalisha.

23. HITIMISHO

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne, Wizara ya Fedha na Uchumi imepata mafanikio makubwa katika jitihada za kukuza uchumi ambapo wastani wa ukuaji wa Pato la Taifa umefikia asilimia 7.2 kwa mwaka pamoja na athari za msukosuko wa uchumi ulioikumba dunia. Pato la la

kila Mtanzania limeongezeka dola za kimarekani 392.8 mwaka 2005 hadi kufikia dola za Kimarekani 517.6 mwaka 2009. Akiba ya fedha za kigeni imewezesha nchi kuwa na uwezo wa uagizaji kwa zaidi ya miezi 5.6, na mapato ya serikali yamezidi sh. 400 bilioni kwa mwezi. Mafanikio yamepatika katika utekelezaji wa MKUKUTA I na changamoto zilizojitokeza zitasaidia kujenga na maandalizi ya MKUKUTA II. Wizara inaendelea kuboresha sheria mbalimbali za kodi na uwekezaji ili kuendelea kuvutia wawekezaji nchini. Jukumu la usimamizi wa matumizi ya fedha za umma lipo mikononi mwa Wizara ya Fedha na Uchumi. Wizara imendelea kusimamia ufanisi na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa ujumla ili kuongeza tija katika matumizi ya fedha za umma.

MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: UKUAJI HALISI WA PATO LA TAIFA (Kwa bei za mwaka 2001)									
	UKUAJI HALISI (%)								
SHUGHULI ZA KIUCHUMI	**2001**	**2002**	**2003**	**2004**	**2005**	**2006**	**2007**	**2008**	**2009[2]**
Kilimo, Uwindaji na Misitu	**4.9**	**4.9**	**3.1**	**5.9**	**4.3**	**3.8**	**4.0**	**4.6**	**2.7**
Mazao	5.3	5.6	3.2	6.6	4.4	4.0	4.5	5.1	2.9
Mifugo	4.0	2.8	2.2	4.1	4.4	2.4	2.4	2.6	2.5
Uwindaji na Misitu	3.6	3.3	3.0	2.7	3.6	4.6	2.9	3.4	1.6
Uvuvi	**4.8**	**6.8**	**6.0**	**6.7**	**6.0**	**5.0**	**4.5**	**5.0**	**3.0**
Viwanda na Ujenzi	**6.6**	**9.4**	**10.9**	**10.9**	**10.4**	**8.5**	**9.5**	**8.6**	**5.6**
Uchimbaji madini na Mawe	13.9	16.9	17.1	16.0	16.1	15.6	10.7	2.5	2.0
Bidhaa za Viwandani	5.0	7.5	9.0	9.4	9.6	8.5	8.7	9.9	6.6
Umeme na Gesi	5.9	6.2	7.2	7.5	9.4	-1.9	10.9	5.4	3.0
Maji	3.5	2.8	4.5	5.2	4.3	6.2	6.5	6.6	5.0
Ujenzi	7.6	11.9	13.8	13.0	10.1	9.5	9.7	10.5	6.3
Huduma	**6.4**	**7.7**	**7.8**	**7.8**	**8.0**	**7.8**	**8.1**	**8.5**	**6.0**
Biashara na Matengenezo	6.4	8.3	9.7	5.8	6.7	9.5	9.8	10.0	6.8
Hoteli na Migahawa	4.8	6.4	3.2	3.6	5.6	4.3	4.4	4.5	1.9
Uchukuzi	4.9	5.9	5.0	8.6	6.7	5.3	6.5	6.9	5.2
Mawasiliano	8.7	10.4	15.6	17.4	18.8	19.2	20.1	20.5	13.5
Fedha	6.9	10.1	10.7	8.3	10.8	11.4	10.2	11.9	7.4
Upangishaji majengo na Huduma za Biashara	4.2	7.1	6.5	6.8	7.5	7.3	7.0	7.1	4.9
Utawala	10.5	9.2	9.6	13.6	11.4	6.5	6.7	7.0	5.2
Elimu	11.4	7.0	2.8	4.0	4.0	5.0	5.5	6.9	5.3
Afya	5.6	8.6	8.7	7.8	8.1	8.5	8.8	9.0	6.9
Huduma nyingine za kijamii na binafsi	3.1	2.1	2.0	3.0	2.6	3.7	3.2	3.1	2.6
Jumla ya Ongezeko la thamani kabla ya marekebisho	6.0	7.2	6.9	7.8	7.4	6.8	7.3	7.5	5.0
Toa ushuru wa huduma za mabenki	2.5	8.7	11.7	10.1	11.8	14.9	15.3	11.0	7.6
Jumla ya ongezeko la thamani kwa bei za mwaka husika	6.0	7.2	6.9	7.8	7.4	6.7	7.2	7.4	5.0
Ongeza kodi katika bidhaa	6.0	7.2	6.9	7.8	7.4	6.8	6.9	7.8	5.7
Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)	**6.0**	**7.2**	**6.9**	**7.8**	**7.4**	**6.7**	**7.1**	**7.4**	**5.0**

[2] Makadirio kwa mwaka 2009

Jedwali Na. 2: Mwenendo wa Ukuaji wa Pato la Taifa Kwa Robo Mwaka, 2006 – 2009

Gross Value Added by Activity Constant 2001 prices – Percentage Changes																				
Year	Quarter	Agriculture	Fishing	Mining and quarrying	Manufac-turing	Electricity	Construc-tion	Wholesale and retail trade	Hotels and restau-rants	Transport and com-munication	Financial interme-diation	Real estate and business services	Public admi-nistration	Education	Other services	FISIM	All indust. at basic prices	Taxes on products	GDP at market prices	GDP, seasonally adjusted
2006	1	3.3	0.5	17.8	13.6	3	25.4	2.3	0.3	22.6	21.4	15.3	8	6.6	6.3	23.7	9.7	10.8	9.8	12.4
	2	6.7	6.4	19.8	10.9	-1.9	10.6	21.1	3.3	6.1	0.6	3.4	6.7	5.6	7	3.1	8.6	9.4	8.7	-14
	3	4	19.9	23.8	7.2	6.2	-0.9	9.7	4.7	0.6	19.7	8.2	5.8	5.3	7.1	18.1	5.9	5	5.8	3.4
	4	-2.2	-5.8	3.5	3.6	14.7	5.8	6.1	8.8	5.5	6	2.2	5.4	2.5	6.8	16	3.7	3.3	3.7	3.3
	Annual	**3.8**	**5**	**15.6**	**8.5**	**5.5**	**9.5**	**9.5**	**4.3**	**8.6**	**11.4**	**7.3**	**6.5**	**5**	**6.8**	**14.9**	**6.9**	**6.8**	**6.9**	
2007	1	3.3	14	17.7	4.6	-1.2	5.9	16.2	3.9	-14.6	-23.2	3.8	6.2	7.1	6.8	-25.3	4.5	-0.3	4.2	3.7
	2	3.5	-7.1	8.6	9.8	4	-1.4	5	4.2	7.4	11.1	15.4	6.8	5	7	15.9	5.7	5	5.7	3.6
	3	5.3	-4.3	5.5	9.1	-3.8	6.2	7.7	6.3	25.8	18.9	2.7	7	3.1	6.9	29.4	6.7	10.1	6.9	-0.4
	4	2	19.1	12	11	-11.1	28.3	11.2	3.3	26.4	31.9	7.6	6.9	6.7	6.7	38	10.4	11.4	10.5	0.9
	Annual	**4**	**4.5**	**10.9**	**8.7**	**-3.3**	**9.7**	**9.8**	**4.4**	**10.1**	**10.2**	**7**	**6.7**	**5.5**	**6.9**	**15.3**	**6.8**	**6.9**	**6.8**	
2008	1	7	-19.4	-0.3	7.4	2.9	7.4	9.6	4.6	16.5	18.8	6.5	7.2	1.7	7.3	25.5	7	8.6	7.1	5.9
	2	5.1	13.3	16.7	5.2	-2.1	-2.3	11.8	3.7	12.9	13.1	7.4	7.9	7.3	6.9	11.7	7	11.5	7.3	-0.5
	3	4.9	30	4.1	10.2	6.2	33.9	12.2	3.5	12.1	11.6	7.8	7.3	8.4	6.9	9.9	9.4	5.7	9.1	1.8
	4	-1.3	-1.2	-9.7	16	15.3	3.5	7.9	6	3.3	7.4	6.8	5.7	10.6	7.1	4.5	5.9	6	5.9	-2.1
	Annual	**4.6**	**5**	**2.4**	**9.9**	**5.6**	**10.5**	**10.2**	**4.5**	**10.8**	**11.9**	**7.1**	**7**	**6.9**	**7**	**11**	**7.4**	**7.8**	**7.5**	
2009	1	0.3	7.9	-40.3	8.8	4.8	9.9	9.3	4.4	13.4	7.9	9.1	4.3	11.5	5.8	7.7	5.4	8.8	5.6	0.5
	2	2.5	6.9	-33.3	11.1	2	8.5	8.6	2.8	16	15.8	6.8	3.4	11.6	5.3	16.9	4.9	1.8	5.2	0.5

Source: National Bureau of Statistics

Jedwali 3: MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI: MWAKA 2009/10 (Julai – Desemba)

shilingi milioni

MAPATO	Bajeti	Makadirio Julai-Desemba	Halisi Julai-Desemba	Halisi kama % ya Makadirio	MATUMIZI	Bajeti	Makadirio Julai-Desemba	Halisi Julai-Desemba	Halisi kama % ya Makadirio
Mapato					**Matumizi Kawaida**				
Mapato ya ndani	5,096,016	2,540,770	2,291,155	90.2%	Mishahara	1,766,388	875,427	840,854	96.1%
Mapato (Serikali za Mitaa)	138,052	69,026	0	0.0%	Matumizi mengine	3,419,842	1,746,226	1,762,136	100.9%
Misaada/Mikopo ya kibajeti	1,193,909	997,264	785,324	78.7%	Mfuko Mkuu (CFS)				
Punguzo la akiba Benki Kuu	506,193	-112,822	78,380	-69.5%	Riba	407,826	160,164	111,200	69.4%
Mikopo - Rollover	576,476	339,262	323,982	95.5%	Madeni (Principal)	651,412	375,130	345,255	92.0%
Kufutiwa madeni MDRI (IMF)	130,635	65,317	13,532	20.7%	Mengineyo	442,786	237,253	166,301	70.1%
Mauzo ya Hisa za Serikali	15,000	15,000	0	0.0%	Marekebisho	0	0	-189,085	
Jumla ndogo	**7,656,282**	**3,913,818**	**3,492,373**	**89.2%**	**Jumla ndogo**	**6,688,254**	**3,394,200**	**3,036,661**	**89.5%**
Miradi ya maendeleo (Nje)	1,857,403	952,852	791,228	83.0%	Miradi ya Maendeleo	2,825,431	1,472,469	1,246,940	84.7%
MCA (T)-USA	211,308	105,654	68,675	65.0%	Fedha za ndani	968,028	519,617	455,712	87.7%
Misaada/Mikopo ya Basket	572,925	310,613	264,021	85.0%	Fedha za nje	1,857,403	952,852	791,228	83.0%
Misaada/Mikopo ya Miradi	1,073,170	536,585	457,229	85.2%	o/w MCA(T)-USA	211,308	105,654	68,675	65.0%
Jumla Kuu	**9,513,685**	**4,866,669**	**4,283,601**	**88.0%**	**Jumla Kuu**	**9,513,685**	**4,866,669**	**4,283,601**	**88.0%**

Jedwali 4: Mwenendo wa Mapato 2005/06 – 2009/10

MWENENDO WA MAKUSANYO YA MAPATO KWA MIAKA 2005/06 HADI 2009/10 (MIL. TSHS.)

									2009/10	
	2005/06		2006/07		2007/08		2008/09			Mapato
		Mapato		Mapato		Mapato		Mapato		Halisi
	Lengo	Halisi	Lengo	Halisi	Lengo	Halisi	Lengo	Halisi	Lengo	Hadi Novemba '09
A. MAPATO YATOKANAYO NA KODI	**1,895,333.0**	**1,946,773.7**	**2,271,137.8**	**2,529,450.0**	**3,189,273.1**	**3,359,280.3**	**4,485,102.0**	**4,044,717.0**	**4,835,410.1**	**1,737,200.7**
1. Ushuru wa Forodha	134,939.7	174,974.3	171,198.3	242,830.9	309,059.7	289,275.6	421,450.0	359,255.3	449,065.4	154,257.5
2. Ushuru wa Bidhaa - Nje	150,347.5	126,507.4	368,310.3	311,984.6	431,653.2	440,272.2	579,917.0	474,782.4	635,131.5	205,736.6
3. Ushuru wa Bidhaa - Ndani	124,818.5	135,042.9	163,059.3	175,954.6	225,011.9	220,616.0	352,004.0	287,243.8	355,982.0	127,280.1
4. Kodi ya Ongezeko la Thamani - Nje	486,300.5	502,437.3	430,891.2	463,753.1	504,929.0	550,289.4	639,331.0	641,458.8	750,652.3	308,171.9
5. Kodi ya Ongezeko la Thamani - Ndani	282,110.1	300,587.3	335,336.2	400,013.7	463,627.1	492,200.4	616,741.0	589,743.0	672,022.8	266,516.3
6. Kodi ya Mapato	544,302.5	539,511.4	624,096.5	717,585.7	827,675.1	983,804.4	1,393,053.0	1,228,642.4	1,443,737.1	476,107.7
7. Kodi Nyingine	172,514.2	167,713.1	178,246.0	217,327.4	427,317.1	382,822.3	482,606.0	463,591.3	528,819.0	199,130.6
B. MAPATO YASIYOTOKANA NA KODI	**171,418.4**	**220,833.1**	**185,857.4**	**238,521.3**	**313,309.9**	**285,725.2**	**244,517.6**	**195,062.6**	**398,658.5**	**87,994.3**
8. Gawio (Parastatal Dividends)	12,072.8	13,232.2	10,317.2	10,542.3	16,122.5	58,253.5	22,449.0	25,865.9	25,597.0	2,767.9
9. Hazina (The Treasury)	43,987.1	73,122.3	42,192.6	67,947.6	98,511.2	44,247.3	20,816.0	13,443.7	34,026.4	5,553.2
10. Wizara Nyingine na Mikoa	115,354.3	134,476.0	133,343.8	160,027.4	198,672.2	183,218.8	201,248.1	155,334.5	200,975.2	79,672.5
11. Maduhuli (Appropriation in Aid)	4.2	2.6	3.8	4.0	4.0	5.6	4.5	418.5	7.6	0.7
12. Mikoa/Wilaya (Regional/District Own Sources)	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	138,052.3	0.0
JUMLA YA MAPATO YA KAWAIDA (A+B)	**2,066,751.4**	**2,167,606.8**	**2,456,995.2**	**2,767,971.3**	**3,502,583.0**	**3,645,005.5**	**4,729,619.6**	**4,239,779.6**	**5,234,068.6**	**1,825,195.0**
13. Ubinafsishaji (Privatization Proceeds)	10,420.0	0.0	4,000.0	0.0	15,000.0	0.0	60,000.0	45,000.0	15,000.0	0.0
JUMLA YA MAPATO YA NDANI	**2,077,171.4**	**2,167,606.8**	**2,460,995.2**	**2,767,971.3**	**3,517,583.0**	**3,645,005.5**	**4,789,619.6**	**4,284,779.6**	**5,249,068.6**	**1,825,195.0**

Jedwali 5: MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE

US $ milioni

	2000 Halisi	2001 Halisi	2002 Halisi	2003 Halisi	2004 Halisi	2005 Halisi	2006 Halisi	2007 Halisi	2008 Matarajio
Urari wa Biashara	**-704.3**	**-709.0**	**-531.7**	**-717.4**	**-1009.7**	**-1321.8**	**-1946.5**	**-2634.0**	**-3403.2**
Zilizouzwa nje (fob)	663.3	851.3	979.6	1216.1	1473.1	1675.8	1917.6	2226.6	3036.7
Zilizonunuliwa toka nje (fob)*	1367.6	1560.3	1511.3	1933.5	2482.8	2997.6	3864.1	4860.6	6439.9
Urari wa Huduma	-52.2	266.1	287.6	222.1	158.9	61.8	278.7	460.3	570.9
Mapato	643.8	915.4	920.1	947.8	1133.6	1269.2	1528.1	1875.7	2168.9
Malipo	696.0	649.3	632.5	725.7	974.7	1207.3	1249.4	1415.4	1598
Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi	-103.9	-152.3	-88.9	-149.1	-119.1	-104.1	-64.1	-58.1	-118.1
Yaliyoingia	50.4	55.3	67.9	87.1	81.8	80.9	80.3	107.3	121.6
Yaliyotoka	154.3	207.6	156.8	236.2	200.9	185.0	144.4	165.4	239.7
Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida	390.8	395.3	431.3	556.9	586.7	496.4	588.7	651.7	617.0
Iliyoingia	463.7	474.8	494.3	619.9	651.7	563.9	654.6	724.0	697.2
Serikalini	427.8	418.4	427.7	553.3	582.0	478.5	559.7	626.9	594.2
Sekta nyingine	35.9	56.4	66.6	66.6	69.7	85.4	94.9	97.1	103
Iliyotoka	72.9	79.5	63.0	63.0	65.0	67.5	65.9	72.3	80.2
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	**-469.6**	**-199.9**	**98.3**	**-87.5**	**-383.2**	**-867.6**	**-1143.2**	**-1580.1**	**-2333.4**
Urari wa Uhamisho wa Mitaji	330.4	1003.6	785.7	692.8	460.0	393.2	5217.7	923.7	637.5
Iliyoingia	330.4	1003.6	785.7	692.8	460	393.2	5217.7	923.7	637.5
Iliyotoka	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Urari katika uwekezaji	572.5	-427.0	255.4	61.2	275.6	807.6	-3954.6	946.1	1915.7
Uwekezaji katika miradi	463.4	467.2	387.6	308.2	330.6	494.1	597.0	647	776.4
Uwekezaji katika hisa	0.0	8.2	2.2	2.7	2.4	2.5	2.6	2.8	2.9
Uwekezaji aina nyingine	109.1	-902.4	-134.4	-249.7	-57.4	311.0	-4554.2	296.3	1136.4
Makosa na Masahihisho	-439.5	-544.0	-806.8	-277.4	-146.3	-555.4	375.0	123.3	111.1
Urari wa Malipo yote	**-6.2**	**-167.3**	**332.6**	**389.1**	**206.1**	**-222.2**	**494.9**	**413.0**	**330.9**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Kuanzia mwaka 2006 bidhaa zilizouzwa nje zinajumuisha pia zile zisizorekodiwa (Unrecorded trade)